# MAJIBU
## YA
# MASWALI MANNE
## YA
# MKRISTO SIRAJUDDIN

Na

Hadhrat Mirza Ghulam Ahmad a.s.

Mwanzilishi wa Jumuiya ya Waislamu Waahmadiyya

Mfasiri

Sheikh Yusufu Athumani Kambaulaya

JUMUIYA YA WAISLAMU WAAHMADIYYA
TANZANIA

ISLAM INTERNATIONAL PUBLICATIONS LTD

Majibu ya Maswali Manne ya Mkristo Sirajuddin

Tafsiri ya Kiswahili ya:

*Siraj-ud-Din 'Isaa'i Ke Chaar Sawaaloń ka Jawaab* (Urdu)

Mtunzi:
Hadhrat Mirza Ghulam Ahmad[as] wa Qadian
Masihi Mau'udi na Imam Mahdi

Mfasiri: Sheikh Yusufu Athumani Kambaulaya

Chapa ya Kwanza ya Kiurdu: Qadian 1897
Chapa ya Kwanza ya Kiswahili: Tanzania 2020
Nakala: 2000

© Islam International Publications Ltd.

Kimeenezwa na:
Jumuiya ya Waislamu Waahmadiyya, Tanzania
Mtaa wa Bibi Titi Mohamed
S.L.P. 376, Dar es Salam.
Simu: +255222110473
Fax: +255222121744

Kimechapwa na:
Ahmadiyya Printing Press, Dar es Salam, Tanzania
Simu: +255222111031

Cover Desgned by: Farhan Naseer

ISBN: 978-1-84880-561-3
10 9 8 7 6 5 4 3 2 1

# Faharisi

*Faharisi*........................................................................3

*Maelezo ya Mwenezi*...............................................................V

*Swali la kwanza* .........................................................................1

*Swali la pili:*..............................................................................33

*Swali la tatu*..............................................................................61

*Swali la nne*...............................................................................71

بِسۡمِ اللّٰہِ الرَّحۡمٰنِ الرَّحِیۡمِ

## Maelezo ya Mwenezi

Bwana Sirajuddin alikuwa Mwislamu na Profesa wa F.C. college, Lahore. Kwa sababu ya kushindwa kujibu maswali ya mapadre akajiunga na Ukristo. Mnamo mwaka 1897 akaja Qadian, kwa siku chache, akakaa na Sayyedna Ahmad a.s., akatambua uzuri wa dini ya Kiislamu na akakiri fadhila yake na akaanza hata kusali. Lakini aliporudi Lahore akajiunga na mapadre tena. Yeye alimwandikia Sayyedna Ahmad a.s. maswali haya manne kutaka majibu yake:

1. Kwa mujibu wa itikadi za Kikristo, kazi maalumu ya Masihi ilikuwa kuja hapa duniani kwa upendo wa mtu na kujitoa dhabihu kwa ajili ya wanadamu. Je, shabaha maalumu ya ujaji wa mwanzilishi wa Islam inaweza kudhihirika katika maana hizi mbili au hapana? Au mbali na upendo na kujitoa dhabihu, je shabaha yake inaweza kuelezwa kwa maneno mengine yaliyo bora zaidi?

2. Endapo shabaha ya lslam ni kuwaleta watu kwenye Umoja wa Mungu, basi ni sababu gani, mwanzoni mwa Islam vita vilipiganwa dhidi ya Mayahudi ambao vitabu vyao havifundishi chochote isipokuwa Umoja wa Mungu? Au kwa nini siku hizi Mayahudi

au wengine wenye kuamini Umoja wa Mungu wafikiriwe kulazimika kusilimu kwa kupata wokovu?

3. Katika Kurani zimo aya gani juu ya kumpenda Mungu na kumpenda mwanadamu, na Mungu kumpenda mwanadamu, ambamo hususan kitenzi cha Upendo na Huba kimetumika?

4. Masihi amesema maneno haya kujihusu: 'Njooni kwangu enyi mliochoka nami nitawapumzisha', na kwamba, 'Mimi ni nuru, na mimi ni njia, mimi ni uhai na ukweli'. Je, mwanzilishi wa dini ya Kiislam aliwahi kusema popote maneno hayo au maneno kama hayo kwa ajili yake mwenyewe?

Mwanzilishi mtukufu wa Jumuiya ya Waislamu Waahmadiyya Sayyedna Ahmad a.s. aliandika majibu ya maswali hayo na kuyaeneza tarehe 22 Juni 1897 kwa faida ya watu wote katika kijitabu kimoja kiitwacho *majibu ya maswali manne ya Mkristo Sirajuddin.*

Kitabu hiki kimetafsiriwa katika lugha ya Kiswahili na Sheikh Yusuf Athumani Kambaulaya, Mbashiri wa Tanzania.

Hapa Makao Makuu katika *deski ya Kiswahili* Maulana Sheikh Jamil R. Rafiq, Mbashiri Mkuu wa zamani wa Tanzania na Kenya, Sheikh Muzaffar Ahmad Durrani, Mbashiri Mkuu wa zamani wa Tanzania na Sheikh Mubarak Mahmud, Mbashiri wa

zamani wa Tanzania waliichunguza tafsiri hii kwa kuilinganisha na matini ya Kiurdu kwa uangalifu sana na kuidurusu.

Aidha ndugu kadhaa wengine nao wakasaidia kwa njia mbalimbali, kama vile Sheikh Ansar Hussain, Sharifu Tanwir Mujtaba na Dkt. Muhammad Shafiq Sehgal.

Hao wote walioshughulikia kazi hii wanastahili kushukuriwa na kuombewa. Mwenyezi Mungu awajaalie malipo bora na Akubali huduma yao. Amin.

Chaudhry Muhammad ‘Ali
Wakilut Tasnif
Tahrik i Jadid
Rabwah. Pakistan
12 Januari, 2010

بِسْمِ اللّٰهِ الرَّحْمٰنِ الرَّحِيْمِ [1]

نَحْمَدُهٗ وَنُصَلِّیْ عَلٰی رَسُوْلِهِ الْکَرِیْمِ [2]

Bwana mmoja aitwaye Sirajuddin aliye Mkristo ameniletea kutoka Lahore maswali manne ili yajibiwe. Nimeonelea kuandika majibu yake na kuyachapisha kwa faida ya wote. Hivyo, maswali yote manne pamoja na majibu yanaandikwa hapa chini.

## Swali la kwanza

Kwa mujibu wa itikadi za Kikristo, kazi maalumu ya Masihi ilikuwa kuja hapa duniani kwa upendo wa mtu na kujitoa dhabihu kwa ajili ya wanadamu. Je shabaha maalumu ya ujaji wa mwanzilishi wa Islam inaweza kudhihirika katika maana hizi mbili au hapana? Au mbali na upendo na kujitoa dhabihu, je shabaha yake inaweza kuelezwa kwa maneno mengine yaliyo bora zaidi?

**Jibu:** Ibainike kuwa muradi hasa unaoonekana wa mwuliza swali hili ni kuwa: jinsi ambavyo sawa na fikara ya Wakristo, Yesu Masihi alikuja duniani ili kwa kuwapenda wenye dhambi ajichukulie laana ya dhambi zao, na kisha auawe kwa sababu ya dhambi

[1] Kwa jina la Mwenyezi Mungu, Mwingi wa rehema, Mwingi wa ukarimu.
[2] Tunamhimidia Yeye na tunamsalia Mtume wake s.a.w.

hizo, je, Kurani nayo inatoa mfano wowote wa dhabihu ya kilaana kwa kuwaokoa wenye dhambi au hapana? Na kama haitoi, basi je, inatoa njia yoyote bora zaidi kuliko hii ili kuwaokoa watu? Kwa kujibu swali hili nasema kuwa Mian Sirajuddin aelewe kwamba Kurani haipendekezi dhabihu yoyote ya kilaana, bali haihalalishi kabisa kuwa dhambi au laana ya mtu mmoja atupiwe mtu mwingine sembuse laana za mamilioni ya watu zikusanywe pamoja na kutiwa shingoni mwa mtu mmoja. Kurani Tukufu inasema wazi wazi kuwa:

لَا تَزِرُ وَازِرَةٌ وِّزْرَ اُخْرٰی [3]

Yaani, mzigo wa mtu mmoja hataubeba mwingine. Lakini kabla sijaeleza mwongozo wa Kurani kuhusu swala la wokovu, naona inafaa niwadhihirishie watu kosa la itikadi hii ya Wakristo, ili mtu anayetaka kulinganisha mafundisho ya Kurani na Injili aweze kulinganisha kwa urahisi.

Basi ibainike ya kuwa fundisho hili la Wakristo kwamba Mungu Aliipenda dunia na ili kuiokoa Akapanga hivi kuwa dhambi za waasi, makafiri na waovu Akamtwisha mwanaye mpendwa Yesu, na kwa kuiokoa dunia katika dhambi Akamfanya mlaaniwa na Akamtundika juu ya mti wa laana, ni fundisho ovu kwa kila jiha na lenye kuaibishwa.

[3] Banii Israaiil 17:16

Ikipimwa kwa mizani ya uadilifu itaonekana ni dhuluma kabisa kwamba dhambi ya Zaid atupiwe Bakari. Dhamiri ya mtu haikubali kabisa kuwa mhalifu aachiliwe, na adhabu ya mhalifu huyo apewe asiyekuwa mhalifu. Na kama uhakika wa dhambi uzingatiwe kulingana na hekima ya kiroho, basi sawa na utafiti huu pia itikadi hii inaonekana mbovu. Kwa sababu, dhambi kwa hakika ni sumu inayozalika wakati mtu anaponyimwa wala hana bahati ya kumtii Mungu na kumpenda Yeye kwa shauku sana na kumkumbuka mwabudiwa kwa mapenzi. Na jinsi ambavyo mti unapong'oka ardhini na kushindwa kunyonya maji, huanza kukauka siku hadi siku na ubichi wake wote hupotea, ndivyo inavyokuwa hali ya mtu ambaye moyo wake huwa umeng'oleka toka kwenye mapenzi ya Mungu; hapo dhambi humtawala kama ukavu. Basi, tiba ya ukavu huu katika kanuni ya tabia ya asili iliyowekwa na Mungu ndiyo kwa njia tatu: (1) Ya kwanza ni upendo (2) Ya pili ni kuomba ghofira ambayo maana yake ni kupenda kufukia na kufunika; kwani maadamu mzizi wa mti unapoimarika katika udongo, huwa na matumaini ya kupata kustawi. (3) Na tiba ya tatu ni toba, yaani kwa kuyavutia maji ya uhai kuelekea kwa Mungu kwa unyenyekevu na kujisogeza karibu naye na kujitoa nje kutoka katika pazia la maasi kwa vitendo vizuri. Na toba siyo kwa ulimi tu, bali toba hukamilika kwa matendo mema. Mema yote ndiyo kwa kukamilisha

toba, kwani shabaha ya hayo yote ni kumkurubia Mungu. Dua pia ni toba kwani kwayo nayo tunatafuta ukaribu na Mungu. Ndiyo sababu Mungu baada ya kuiumba nafsi ya mtu Akaiita roho, kwani raha yake ya kweli na starehe imo katika kumwamini Mungu na kumpenda na kumtii Yeye. Akaipa jina *nafs,*[4] kwani hiyo huungana na Mungu. Kuungana na Mungu mfano wake ni kama mti uliopo ndani ya bustani ambao unaimarika vizuri katika ardhi ya bustani. Hiyo ndiyo pepo ya mwanadamu. Na kama vile mti unavyokunywa maji ya ardhi na kuyavuta ndani mwake na kwayo hutoa nje gesi zenye sumu, hivyo ndivyo ilivyo hali ya moyo wa mtu; huo nao baada ya kunywa maji ya huba ya Mungu hupata nguvu ya kutoa nje takataka zenye sumu na kuzitupilia mbali hizo kwa urahisi, na ukiwa ndani ya Mungu huendelea kukua kwema na kupanuka sana na kustawi vizuri na kutoa matunda mazuri. Lakini moyo usiofungamana na Mungu hauwezi kunywa maji yenye kukuza hivyo, huendelea kukauka saa zote; mwishowe majani nayo hupukutika na matawi makavu yachukizayo macho yanabaki. Basi, kwa kuwa unyaufu wa dhambi hutokana na kutokuwa na uhusiano (na Mwenyezi Mungu), hivyo tiba sahihi ya kuuondoa unyaufu huo ni uhusiano imara (na Mwenyezi Mungu). Utaratibu wa ulimwengu

[4] Katika lugha, *Nafs* inamaanisha kitu chenyewe. *Mwandishi.*

hulishuhudia jambo hili. Mungu Mwenye shani Akiashiria kwenye habari hiyo Anasema:

يَٰٓأَيَّتُهَا ٱلنَّفۡسُ ٱلۡمُطۡمَئِنَّةُ ٢٨ ٱرۡجِعِيٓ إِلَىٰ رَبِّكِ رَاضِيَةٗ
مَّرۡضِيَّةٗ ٢٩ فَٱدۡخُلِي فِي عِبَٰدِي ٣٠ وَٱدۡخُلِي جَنَّتِي ٣١[5]

Yaani, Ewe roho uliyepata faraja kutoka kwa Mungu, rudi kwa Mola wako hali ya kuridhika na kumridhisha. Basi ingia katika watumishi Wangu, na ingia katika pepo Yangu.

Ilimuradi, tiba ya kuondoa dhambi ni huba ya Mungu na upendo wake tu. Hivyo, amali zote njema zinazotoka katika chemchem ya huba na upendo humwagilia maji moto wa dhambi; kwani, mtu anathibitisha upendo wake kwa kutenda mwema kwa ajili ya Mungu. Kumwamini Mungu katika maana ya kumtanguliza juu ya kila kitu hata juu ya nafsi yake pia, ndiyo daraja ya kwanza ya upendo ambayo inafanana na ile hali ya mti ambapo mti huo unapandwa ardhini. Na kisha daraja ya pili ni *istighfar* ambayo muradi wake ni kwamba aibu zake zisionekane kwa kutengana na Mungu; na daraja hii inafanana na ile hali ya mti ambapo mti huo unaimarisha kwa nguvu mzizi wake ardhini kikamilifu. Na daraja ya tatu ni toba ambayo inafanana na ile hali ambapo mti kwa kusogeza mizizi yake karibu ya maji unayanyonya kama mtoto

[5] Al-Fajr 89: 28-31

anavyonyonya. Ilimuradi, hekima ya dhambi ndiyo hii kwamba hiyo inazalika kwa kutengana na Mungu. Hivyo, kuiondoa kunakutegemea kufangamana na Mungu. Basi, ni wajinga walioje wale ambao wanasema kwamba kujiua kwa mtu ni tiba ya dhambi.

Ni jambo la kichekesho kwamba ili kumhurumia mwingine anayeumwa kichwa, mtu ajipige jiwe kichwani, au kwa kumwokoa mwingine ajiue. Nadhani hakuna mwenye akili duniani anayeweza kufikiri kuwa kujiua hivyo ndiyo kumhurumia binadamu. Hamna shaka kwamba kumhurumia binadamu ni jambo zuri, na kusumbuka kwa kuwasalimisha wengine ndiyo kazi ya mashujaa, lakini, je, hii ndiyo njia ya kuvumillia taabu inayosemekana kumhusu Yesu? Laiti Yesu angelijiepusha kujiua, bali angelivumulia taabu kwa njia ya akili kama wenye busara ili kuwaletea raha wengine, ndipo dunia ingeweza kunufaika naye. Kwa mfano, mtu mmoja maskini anahitaji nyumba, lakini hana uwezo wa kumwajiri mwashi, basi kama mwashi mmojawapo akimhurumia huyo anashughulikia kwa kuvumilia shida sana kwa siku chache kumjengea nyumba bila kudai ujira, hapo mwashi huyo bila shaka atastahiki sifa. Na bila shaka amemfanyia hisani maskini kwa kumjengea nyumba. Lakini kama huyo kwa kumhurumia maskini ajipige

jiwe kichwani, hapo maskini atapata faida gani? Ni masikitiko kuwa wako watu wachache sana duniani wanaofuata njia za kiakili za kutenda wema na kuhurumia. Kama ni kweli kwamba Yesu kwa hakika alijiua akifikiria watu watapata kuokoka kwa kufa kwangu, basi hali ya Yesu inastahili kuhurumiwa sana; na tukio hili halistahili kuelezwa, bali lafaa kufichwa.

Na tukichunguza fundisho hili la Wakristo kulingana na maana ya laana iliyopendekezwa kwa Yesu, tunalazimika kusema kwa kusikitika sana kuwa Wakristo kwa fundisho hilo wamemvunjia Yesu heshima kwa namna ambavyo hakuna taifa lolote duniani lililomwunjia hivyo heshima Mtume au Nabii wake. Kwa maana, Yesu kuwa mlaaniwa, angalau kwa siku tatu tu, ndiyo sehemu ya imani ya Wakristo. Na kama Yesu asifanywe mlaaniwa, basi sawa na itikadi ya Wakristo kafara na kujitoa dhabihu yote hubatilika. Ndiyo kusema kwamba nguzo ya itikadi hii yote ndiyo laana.

Na mambo haya kwamba alitumwa duniani kwa kuwapenda wanadamu na akajitoa dhabihu kwa ajili ya watu, haya yote sawa na fikara ya Wakristo yanafaa sharti iaminiwe kwamba kwanza Yesu akawa mlaaniwa kwa dhambi za dunia, na kisha akawambwa juu ya mti wa laana. Ndiyo maana tumekwisha dokeza hapo awali kuwa dhabihu ya Yesu ni dhabihu

ya kilaana. Dhambi imeleta laana na laana ilisababisha msalaba. Sasa jambo la kuamuliwa ni hili kwamba je, laana inaweza kunasibishwa kwa mtu mnyofu? Basi iwe wazi kwamba Wakristo wamefanya kosa kubwa kwamba walihalalisha kutumia neno laana kwa Yesu, hata kama ni kwa siku tatu tu au siku chache kuliko hizi. Kwa maana, laana huhusikana na moyo wa mtu maluuni; na mtu huitwa maluuni ambapo moyo wake unatengana na Mungu, na unakuwa adui wake. Ndiyo maana, *Laiin* (mlaaniwa) ni jina la shetani. Na ni nani asiyejua kwamba kulaani ndiyo kufukuzulia mbali kutika daraja la ukaribu. Na neno hili linatumika kwa mtu ambaye moyo wake umekuwa mbali na upendo na utii wa Mungu naye amekuwa kweli adui wa Mungu. Hiyo ndiyo maana ya neno laana waliyokubaliana wataalamu wote wa lugha. Sasa tunahoji, kama kweli Yesu Masihi akalaaniwa, basi, hakuna budi yeye kwa hakika akaghadhibikiwa na Mungu, na utambuzi wa Mungu na utii na upendo wake ukatoweka moyoni mwake, na Mungu akawa adui wake, naye akawa adui wa Mungu, Mungu Akamchoka yeye, naye akamchoka Mungu kama ilivyo maana ya laana. Basi inalazimika kwamba katika siku za laana, kwa hakika, yeye alikuwa kafiri, mbali na Mungu na adui wake, na alikuwa na hisa ya shetani ndani yake. Basi, kuamini hivyo kuhusu Yesu –Mungu apishe mbali— ndiyo kama kumfanya yeye kuwa ndugu wa Shetani.

Nafikiri, mcha-Mungu yeyote hatajasiri kuamini hivyo kuhusu nabii mmoja mnyofu, isipokuwa tu mtu habithi na mwenye tabia chafu.

Basi, kama neno hili limekuwa batili kwamba kwa hakika moyo wa Yesu Kristo ulilaaniwa, itabidi kuamini papo hapo kuwa dhabihu hiyo ya kilaana pia ni batili na ni mpango wa wajinga wenyewe. Kama wokovu unaweza kupatikana hivi tu kwamba kwanza Yesu ahesabiwe shetani, mbali na Mungu na aliyemchoka Mungu, basi ulaaniwe wokovu wa aina hii!!! Ingekuwa afadhali kama Wakristo wangekubali jahanamu kwa ajili yao, lakini wasingempachika aliyemkurubia Mungu lakabu ya shetani. Ni sikitiko kwamba watu hawa wameyategemea mambo ya kipuuzi na machafu. Upande mmoja wanamdhania kuwa mwana wa Mungu na aliyetoka katika Mungu, na aliyeungana na Mungu, na upande wa pili wanampa lakabu ya shetani, kwani laana inahusikana na shetani, na *Laiin* (mlaaniwa)ni jina la shetani, na mlaaniwa ni yule aliyetoka katika shetani na aliyeungana na shetani, na mwenyewe ndiye shetani. Basi, kulingana na itikadi za Wakristo ndani ya Yesu kuna Utatu wa aina mbili: wa Kirahmani na wa Kishetani. Na Mungu apishe mbali, Yesu akiwa ndani ya shetani akajiunganisha na shetani na kwa njia ya laana akajipatia sifa za kishetani, yaani akamwasi Mungu, akamchoka Mungu, akawa adui wa Mungu.

Sasa hebu bwana Sirajuddin, sema kwa uadilifu kuwa je, kazi kubwa inayonasibishwa kwa kristo ina utakaso wowote wa kiroho au wa kiakili? Je, katika dunia kutakuwa na itikadi yoyote mbaya zaidi kuliko hii kuwa mkweli mmoja achukuliwe kuwa adui wa Mungu, na mwasi wa Mungu, na shetani ili kujipatia wokovu? Je Mungu Mweza na Mrehemevu na Mkarimu Alikuwa na haja gani ya dhabihu hii ya kilaana?

Kisha jambo hili linapoangaliwa kwa jiha hii kwamba je, fundisho hili la dhabihu ya kilaana walipewa Mayahudi pia au hapana, hapo uwongo wake unazidi kudhihirika. Kwani, ni wazi kwamba endapo Mwenyezi Mungu Alikuwa na njia hii tu moja ya wokovu mkononi mwake ya kuwa Yeye Awe na mwana mmoja, naye huyo abebe laana ya wote wenye dhambi na kisha akiwa dhabihu ya kilaana awambwe msalabani, hapo ilikuwa lazima kwamba kwa Mayahudi ndani ya Torati na vitabu vingine vilivyo mikononi mwa Mayahudi dhabihu hiyo ya kilaana ingepata kutajwa. Kwani yeyote mwenye akili hawezi kukubali kwamba kanuni ya Mungu ya tangu azali na ya milele Aliyoiweka kwa ajili ya wokovu wa wanadamu iendelee kubadilika daima; iwe moja katika zama za Torati na iwe nyingine katika zama za Injili, na iwe tofauti tena katika zama za Kurani; na iwe tofauti kabisa kwa ajili ya Manabii waliokuja

katika sehemu nyingine za dunia. Sasa tunapofanya utafiti na uchunguzi, yabainika kwamba katika Torati na vitabu vyote vya Mayahudi mafundisho ya dhabihu ya kilaana hayamo. Kwa hiyo, tuliwaandikia siku hizi barua wanazuoni maarufu wa Kiyahudi na tukawauliza kwa yamini ya Mwenyezi Mungu kuwa ndani ya Torati na vitabu vingine mmepewa mafundisho gani kwa ajili ya wokovu wa wanadamu? Je, mmefundishwa kuiamini kafara ya mwana wa Mungu na kujitoa kwake dhabihu? Au kuna mafundisho mengine? Nao wakajibu kuwa fundisho la Torati kuhusu wokovu linalingana kabia na fundisho la Kurani, yaani kumuelekea Mungu kwa ukweli wa moyo na kuomba msamaha wa dhambi, na kwa kujiepusha na tamaa za nafsi kutenda mema kwa kupata radhi ya Mungu, na kutekeleza kwa nguvu na kukazania mipaka yake, kanuni zake maamrisho yake na wasia wake. Hii ndiyo njia ya kupata wokovu iliyotajwa mara kwa mara katika Torati ambayo manabii watukufu wa Mungu waliendelea kuwalazimisha wafuasi wao kuifuata, na ambayo kwa kuiacha adhabu pia ziliendelea kushuka. Na wanazuoni hao wa Kiyahudi hawakuishia tu kunijibu kwa barua za maelezo marefu, bali wakanitumia vitabu vya wahakiki wao wataalamu vinavyopatikana kwa nadra na ambavyo havina kifani, vilivyoandikiwa juu ya swala hilo, ambavyo ninavyo mpaka sasa, na barua pia zipo. Atakaye kuviona

naweza kumwonyesha; nakusudia kuandika barua hizo zote katika kitabu kimoja chenye maelezo kamili.

Sasa mwenye akii anapaswa kufikiria kwa uadilifu kabisa na moyo safi kwamba kama hii ndiyo kweli kuwa Mwenyezi Mungu Akiisha mpanga Yesu Kristo mwana na kwa kumtwisha laana za wengine Akaifanya dhabihu hii ya kilaana kuwa njia ya wokovu wa watu, na fundisho hilo ndilo walilopewa Mayahudi, basi kwa nini Mayahudi waliyaficha mafundisho hayo mpaka leo, na wakadumu kukazania kuwa maadui zake? Na hoja hii inapata nguvu zaidi tuonapo kuwa manabii walifululiza kuja kujadidisha mafundisho ya Mayahudi, na Hadhrat Musa a.s. akayaeleza mafundisho ya Torati mbele ya malaki ya watu, basi iliwezekanaje Mayahudi wasahau mafundisho hayo yaliyofululiza kufundishwa na manabii, ilhali waliamriwa waandike amri za Mungu na wasia wake kwenye miimo ya malangu na malango na kwenye mikono ya nguo zao, na wawafundishe watoto wao na wenyewe wayahifadhi kwa moyo. Sasa, je, hili laweza kueleweka akilini, au dhamiri safi ya mtu yeyote inaweza kutoa ushahidi, kwamba pamoja na nyenzo zote za uangalizi kuwepo, madhehebu yote ya Mayahudi yakayasahau mafundisho mazuri ya Torati yaliyokuwa tegemeo la wokovu wao. Mayahudi sio leo bali tangu zamani wameendelea

kusema kwamba katika Torati mambo yale yale yameelezwa kuwa njia ya wokovu yaliyoelezwa katika Kurani kuwa njia ya wokovu. Basi walitoa ushahidi huo wakati Kurani ilipoteremka na hata sasa pia wanatoa ushahidi huo huo, na juu ya madhumuni hayo barua zao na vitabu vimeniwasilia. Kama Mayahudi wangekuwa wamepewa mafundisho ya dhabihu ya kilaana kwa kupata wokovu, basi haijulikani sababu kwa nini wangeyaficha mafundisho hayo. Naam, iliwezekana wasingemwamini Yesu Kristo kuwa mwana wa Mungu wala wasingechukulia kusulubiwa kwake kuwa kusulubiwa kwa Mwana wa kweli, na wangesema kuwa mwana wa kweli ambaye kwa dhabihu yake dunia itapata wokovu si huyu, bali huyo atadhihiri katika zama nyingine katika siku zijazo. Lakini haingewezekana kwa vyovyote kuwa madhehebu yote ya Mayahudi yangekana mafundisho yaliyokuwa ndani ya vitabu vyao, na ambayo Manabii watukufu wa Mungu waliendelea kuyafundisha upya. Mayahudi wapo mpaka sasa na wanazuoni na maulamaa wao nao wapo na vitabu vyao pia vipo. Kama yeyote ana shaka, basi awaulize ana kwa ana. Je, mwenye akili ambaye kwa kweli anatafuta haki hahitaji kupata ushahidi wa Mayahudi pia katika jambo hili. Je, Mayahudi sio mashahidi wa kwanza walioendelea kuhifadhi kwa moyo mafudisho ya Torati tangu mamia ya miaka? Kumfanya mtu mmoja mnyonge

kuwa Mungu pasipokuwa na ushahidi wa mafundisho ya zamani wala ushahidi wa warithi wa mafundisho hayo, wala ushahidi wa mafundisho ya badaaye, wala ushahidi wa akili, na kumwita mtu huyo kuwa wa Mungu na tena wa shetani pia, je, kuyaamini mafundisho hayo machafu yasiyoingia akilini ni kazi ya watu wenye asili safi!!

Kisha inapoangaliwa itikadi hiyo kwa jiha hii kwamba ingawaje mafundisho ya Torati yaliyorithiwa na yale ya zamani yalipingwa, na dhambi ya mmoja akatupiwa mwingine, na moyo wa mnyofu mmoja ukahesabiwa kuwa mlaaniwa, kuwa mbali na Mungu na kuachwa na Mungu, na kuwa mwenziye shetani, lakini pamoja na mabaya hayo yote wakanufaika nini wenye kukubali dhabihu hii ya kilaana — je, wakaacha kutenda dhambi au wakasamehewa dhambi zao — hapo unazidi kuthibitika ubovu wa itikadi hiyo. Kwani, wao kuacha dhambi na kupata utakaso wa kweli ni kinyume waziwazi na uhakika ulivyo. Maana, sawa na imani ya Wakristo, hata Nabii Daudi a.s. pia aliiamini kafara ya Yesu, lakini, wasemavyo baada ya kuiamini, Mungu Apishe mbali, Hadhrat Daudi a.s. akamwua mtu mmoja asiyekuwa na hatia na kufanya zinaa na mke wa huyo jamaa. Na kwa ajili ya mambo ya anasa alitumia mali ya hazina ya Ukhalifa na akaoa wanawake mpaka mia moja. Na Hadi mwisho wa uhai wake, akaendelea kurudia

kufanya madhambi. Na kila siku alitenda dhambi kwa ujasiri mkubwa. Hivyo, kama dhabihu ya kilaana ya Yesu ingeweza kuzuia kufanye dhambi, basi sawa na kauli yao Daudi asingezama katika maasi kiasi hicho. Vile vile mabibi watatu wa Yesu walitenda maasi ya zinaa. Kwa hiyo ni dhahiri kuwa kuamini dhabihu ya kilaana ya Yesu ingekuwa na athari ya kuleta utakaso wa ndani, basi mabibi wake lazima wangenufaika kwayo na wasingepata kutenda dhambi kama hizo za aibu. Kadhalika wanafunzi wa Yesu pia baada ya kuamini wakatenda dhambi zenye aibu. Yuda Iskariote alimwuza Yesu kwa vipande thelathini vya fedha na Petro akamlaani Yesu mara tatu akisimama mbele yake na wengine wote wakamkimbia. Na ni dhahiri kuwa kumlaani Nabii ni dhambi kubwa sana. Na dhorubu ya unywaji wa pombe na uzinzi inayoipiga Ulaya siku hizi haina haja ya kuandika. Tumekwisha eleza katika toleo moja la zamani habari za uzinzi wa mapadre wakubwa kwa kutaja marejeo ya magazeti ya huko Ulaya. Matukio hayo yote yanathibitisha kwa uwazi kuwa dhabihu hiyo ya kilaana haikuweza kuzuia dhambi.

Sasa, jiha ya pili ni hii kwamba kama dhambi haziwezi kuzuiwa, basi je, kwa dhabihu hii ya kilaana dhambi zinasamehewa sikuzote! Kana kwamba hili ndilo agizo ambalo kwalo mhuni mmoja baada ya kumwua mtu pasipo haki, au kuiba, au kuharibu mali

au maisha au heshima ya mtu kwa kutoa ushahidi wa uwongo, au kujitwalia mali ya mtu aliyowekewa amana, na kisha kwa kuamini dhabihu hii ya kilaana anaweza kuchukua haki za watu wa Mungu. Kadhalika akikaa sikuzote katika hali chafu ya kufanya uzinzi, anaweza kuepuka na adhabu kali ya Mwenyezi Mungu kwa kukiri tu dhabihu ya kilaana. Basi, ni dhahiri sana kwamba sivyo ilivyo kabisa. Bali, baada ya kutenda maasi kisha kuingia chini ya kivuli cha dhabihu ya kilaana ni desturi ya kihuni. Na inaonekana Paulo pia alianza kupata wasiwasi kwamba kanuni hii si sahihi, ndiyo maana akasema, “Dhabihu ya Yesu ni kwa ajili ya dhambi ya kwanza na Yesu hawezi kusulubiwa mara ya pili.” Lakini kwa kauli hii amenasa katika matatizo mazito sana. Kwani kama ni sahihi kuwa dhabihu ya kilaana ya Yesu ni kwa ajili ya dhambi ya kwanza, basi, kwa mfano, Nabii Daudi, Mungu Apishe mbali, atapaswa kukaa jahanamu ya milele, kwani sawa na usemi wa Wakristo alimzini mke wa Uria, na kisha bila ruhusa ya Mungu akakaa naye maisha yote, na huyo ndiye bibi mtukufu wa Yesu katika mfululizo wa mama za Mariamu. Isitoshe, Daudi alioa wake mpaka mia, jambo ambalo halikumpasa kulifanya kwa mjibu wa ikirari ya Wakristo. Basi, dhambi hiyo haikubakia kuwa ya kwanza bali iliendelea kufanyika mara kwa mara, na kila siku ikarudiwa upya. Tena, kama dhabihu ya kilaana haiwezi kuzuia dhambi, basi bila

shaka dhambi zitakuwa zinatendwa na Wakristo wa kawaida pia kama zinavyoendelea kutendeka hata hivi sasa. Basi kwa mujibu wa kanuni ya Paulo haistahili kusamehewa dhambi yao ya pili, na adhabu ya Paulo haistahili kusamehewa dhambi yao ya pili, na adhabu yake ni jahanamu ya milele. Katika hali hii hata Mkristo mmoja hathibitiki kuwa mwenye kujiokoa katika jahanamu ya milele. Kwa mfano, Mian Sirajuddin asiende mbali, bali aangilie hali yake mwenyewe kwamba kwanza alimwamini mwana wa Mariamu kuwa mwana wa Mungu akapata ubatizo wa dhabihu ya kilaana, kisha akaja Qadian akasilimu upya, akakiri kuwa alifanya haraka kupata ubatizo. Na aliendelea kusali na mara nyingi alikiri mbele yangu kuwa ubovu wa kafara umebainika kwangu nami naiona kuwa batili. Kisha alipoondoka Qadian kwenda kwao, huko akaghilibiwa na Mapadre na akatanasari. Sasa, yampasa Mian Sirajuddin afikirie mwenyewe kwamba kwanza alipoiacha dini ya Kikristo baada ya kupata ubatizo na akaipinga kwa maneno na matendo yake, basi kwa kanuni ya Ukristo hiyo ilikuwa dhambi kubwa aliyoitenda mara ya pili. Basi sawa na kauli ya Paulo dhambi yake hii haitasamehewa, kwani hiyo yahitaji (Yesu) kusulubiwa mara ya pili.

Na kama mseme Paulo amekosea au ameongopa, na ukweli wenyewe ni kuwa baada ya kuamini dhabihu

ya kilaana dhambi haiwi dhambi tena — ibeni, zinzini, ueni bila haki, semeni uwongo, fanyeni hiana katika amana; ilimuradi, fanyeni chochote hamtaadhibiwa kwa dhambi yoyote — basi, dini ya namna hii itakuwa dini ienezayo unajisi. Na serikali yapaswa kuchukua dhamana kutoka kwa wenye itikadi za namna hii. Na kama mkikariri wazo hili tena kuwa anayeiamini dhabihu ya kilaana hupata utakaso wa kweli na huondokana na dhambi, basi, tumesha lijibu mapema kuwa jambo hili si sahihi hata kidogo. Na tumeshaandika sasa hivi dhambi ya Nabii Daudi, dhambi za bibi za Yesu, na dhambi za wanafunzi wake, na dhambi za waheshimiwa mapadri. Na wote wenye uzoefu wanafahamu kuwa siku hizi Ulaya ndiyo ya kwanza katika viranga. Ikiwa mfano wa maisha matakatifu ya mtu fulani utajwe, basi kuna uthibitisho gani kwamba kweli maisha yake ni matakatifu? Waovu wengi, wala haramu, wazinifu, wasio na ghera, walevi na wakana Mwenyezi Mungu wanaweza kujifanya watakatifu, lakini kwa undani wao ni kama makaburi ambamo hamna chochote isipokuwa maiti inukayo na mifupa yake.

Zaidi ya hayo, haifai kudhania kwamba watu wote wa taifa fulani ni wema kiasili au wote ni waovu kiasili. Bali tunaona kwamba kanuni ya asili ya Mungu imelipatia kila taifa haki ya kudai kwamba kama ambavyo miongoni mwake wapo watu walio kiasili

wenye hulka mbaya na tabia mbovu na wenye kuwatakia wengine ubaya na wenye mienendo mibaya, ndivyo wanavyokuwapo kinyume chao baadhi ya watu wengine walio kiasili wapole, wenye hulka njema, tabia njema na wenye mienendo mizuri. Katika kanuni hii ya kiasili hawako nje hata Mabaniani, wala Waparsi, wala Mayahudi, wala Makalasinga wala wafuasi wa dini ya Bud'ha; hata matopasi na wenye hadhi ndogo katika jamii (ya kibaniani) pia wanaingia katika kanuni hii. Kadiri watu wanavyosonga mbele katika ustaarabu na kuendelea kupata heshima na elimu na staha, ndivyo watu wao wenye tabia nzuri wanavyopata sifa nzuri katika maisha yao safi na mienendo mizuri na kuonesha mfano wao mzuri kwa mng'ao sana. Kama baadhi ya watu katika mataifa yote wasingekuwa na kipawa cha wema katika tabia ya asili, basi kipawa hicho kisingeweza kuzalika hata kwa kubadili dini; maana, tabia ya asili iliyoumbwa na Mungu haibadiliki. Kama mtu ana kiu ya kupata ukweli basi atalazimika kukubali kuwa kabla ya kuwepo dini, tabia zimekwisha kasimiwa na Mungu hivi kwamba katika tabia ya mtu mmoja kuna upole na upendo mwingi zaidi, na katika tabia ya mwingine kuna ukali na hasira nyingi mno. Sasa, dini inafundisha kwamba ule upendo, utii, unyofu, na uaminifu ambao, kwa mfano, mwabudu masanamu au mwabudu binadamu anaonyesha kuhusu kiumbe kwa sura ya ibada,

azielekeze nia hizo kwa Mungu na utii ule aonyeshe katika njia ya Mungu.

Ama swali hili kuwa dini inaleta badiliko gani katika maumbile ya mwanadamu, Injili haijatoa jibu lake lolote, maana Injili iko mbali na njia za hekima. Lakini Kurani Tukufu mara nyingi inatatua tatizo hili kinaganaga kwamba dini haina madaraka ya kugeuza maumbile ya kiasili ya wanadamu, na kumgeuza mbwa mwitu kuwa mbuzi. Bali shabaha kuu ya dini ni hii tu kwamba yale maumbile na vipawa vilivyomo kiasili katika mwanadamu, dini iongoze kuvitumia hivyo katika mahali pafaapo. Dini haina uwezo wa kubadili nguvu yoyote ya kiasili. Naam, inao uwezo huu kwamba iongoze kwa kuitumia katika mahali pafaapo, na isitilie mkazo nguvu moja tu, mathalan isikazanie huruma au msamaha tu bali iagize kuzitumia nguvu zote. Kwani, miongoni mwa nguvu za kibinadamu hakuna nguvu yoyote iliyo mbaya, bali ubaya wenyewe ni kupunguza na kuzidisha na kuitumia vibaya. Na mtu anayestahili kulaumiwa, hastahili kulaumiwa kwa sababu ya nguvu za kiasili, bali kwa sababu ya kuzitumia vibaya anastahili kulaumiwa. Ilimuradi, Mgawaji mwenye madaraka kamili Amelipatia kila taifa nguvu za kiasili kwa usawa. Na kama watu wa mataifa yote walivyopewa pua, macho, kinywa, mikono na miguu na viungo vinginevyo vya dhahiri, ndivyo walivyojaaliwa nguvu

za ndani pia. Kwa kuangalia watumiao nguvu zao kiwasitani au kidogo sana kabisa au kupita kiasi, katika kila taifa wapo watu walio wema na pia wabaya. Lakini taifa fulani kuwa jema kwa kuathirika na dini, au kusema kuwa dini fulani ndiyo sababu hasa ya ustaarabu wa taifa fulani, kutathibitika hapo tu ambapo zipatikane katika baadhi ya wafuasi wakamilifu wa dini ile sifa kamilifu za kiroho ambazo mfano wake usipatikane katika dini nyingine. Kwa hiyo, nasema kwa nguvu kuwa sifa hiyo imo ndani ya Islam. Islam imewafikisha maelfu ya wafuasi wake kwenye daraja ile ya maisha matakatifu ambamo twaweza kusema kuwa kana kwamba roho ya Mungu inakaa ndani yao. Mwanga wa kukubaliwa na Mungu umezalika ndani yao kana kwamba hao ndio mahali pa Mungu kujidhihirisha. Watu hao wameendelea kupatikana katika kila karne; na maisha yao matakatifu siyo bila dalili, wala siyo madai matupu, bali Mungu Ameendelea kutoa ushahidi kuwa maisha yao ni matakatifu.

Ikumbukwe kwamba Mwenyezi Mungu ameeleza katika Kurani Tukufu alama ya maisha matakatifu ya daraja ya juu ndiyo kwamba maajabu yanadhihiri kwa mtu huyo, na Mwenyezi Mungu hupokea dua ya watu hao, na Huzungumza nao, na huwajulisha habari za ghaibu kabla hazijatokea na Huwasaidia. Basi, twashuhudia kwamba maelfu ya watu wa aina hii

wameendelea kuwepo katika Islam. Na katika zama hizi nipo mimi ili kuonyesha mfano huu. Lakini, wako wapi watu wa aina hiyo baina ya Wakristo na wanakaa katika nchi gani ambao sawa na alama zilizoelezwa ndani ya Injili wanaweza kuthibitisha imani yao ya kweli na maisha yao matakatifu? Kila kitu hutambulikana kwa alama zake, kama vile kila mti hutambulikana kwa matunda yake. Na kama ni madai matupu tu ya maisha matakatifu, lakini alama zilizowekwa ndani ya vitabu vyao hazitoi ushahidi juu ya ukweli wa madai hayo, basi hayo madai ndiyo batili. Je, Injili haikuandika alama yoyote ya Imani barabara ya kweli? Je, hiyo haikueleza alama hizo kuwa ni kama miujiza? Hivyo, kama ndani ya Injili alama za waumini wa kweli zimeandikwa, basi kila Mkristo adaiye ana maisha matakatifu anapaswa kujaribiwa sawa na alama za Injili. Hebu linganisheni kati ya Padri mmoja mtawa sana na Mwislamu mmoja masikini kabisa katika kujaliwa mwanga wa kiroho na kukubaliwa na Mungu, kisha kama padri huyo akipatikana na sehemu yoyote iwayo ya mwanga wa kimbinguni ndani yake kwa kulinganishwa na Mwislamu huyo maskini, basi tutastahili kupewa kila adhabu. Ndiyo maana, mara kadhaa nimeshatangaza kuhusu jambo hili kwa Wakristo. Nami nasema kweli kabisa, na Mungu wangu ndiye shahidi, kuwa imethibitika kwangu kwamba imani ya kweli na maisha matakatifu hasa

yanayopatikana kwa nuru ya kimbinguni hayawezi kupatikana kwa njia yoyote isipokuwa Islamu. Maisha haya matakatifu tuliyojaaliwa sisi, siyo majisifu tu ya midomo yetu, bali kuna ushahidi wa kimbinguni juu yake. Maisha matakatifu yoyote hayawezi kuthibitika bila ushahidi wa kimbinguni, wala hatuwezi kujua unafiki wa mtu uliofichika na kutoamini kwake. Naam, wanapokuwapo watu wenye nyoyo safi walio na ushahidi wa kimbinguni katika taifa fulani, hapo watu waliosalia wa taifa hilo waonekanao wenye maisha matakatifu kidhahiri nao watahesabiwa kuwa wenye maisha matakatifu, kwani taifa ni kama mwili mmoja, na kwa mfano mmoja pekee yaweza kuthibitika kuwa taifa hili linaweza kupata maisha matakatifu kimbinguni.[6]

Ndiyo sababu nilitoa tangazo likatalo shauri kwa Wakristo. Basi, kama wangekuwa watafuta ukweli wangelitia maanani. Na ninasema hata sasa kwamba Wakristo pia wanadai kuwa na imani na maisha yaliyotakasika na Waislamu kadhalika. Sasa jambo la kuamuliwa ni hili kuwa kati ya makundi haya mawili ni kundi gani ambalo imani yake inakubaliwa mbele ya Mungu nalo lina maisha matakatifu kwa kweli, na imani ya lipi ni mawazo tu ya kishetani na madai yake ya maisha mema ni udanganyifu uliosababishwa

[6] Tanbihi: Hapa kuelezea kisa fulani cha zamani ni upuuzi; yafaa kuonyesha matukio ya sasa katika mkabala. *Mwandishi.*

na upofu. Basi, nionavyo mimi, imani ambayo ina ushahidi mwingi wa kimbinguni na ina alama za kukubaliwa na Mungu ndiyo imani sahihi na ya kukubaliwa. Kadhalika, na maisha matakatifu kwa kweli ndiyo yale yaliyo na alama za kimbinguni. Kwa sababu, kama ni kukubali madai tu, basi mataifa yote ya duniani yanadai kuwa kati yetu wamepita watu wengi wenye maisha safi na wapo pia hata sasa; bali husimulia amali na matendo yao pia ambayo kuamua uhakika wa ndani ni vigumu. Kwa hiyo, kama Wakristo wanadhani kuwa imani safi na maisha matakatifu hupatikana kwa sababu ya kafara, basi wanawajibika wajitokeze sasa uwanjani kushindana nami katika kukubaliwa maombi na kudhihiri ishara. Kama kwa ishara za kimbinguni maisha yao yakithibitika kuwa matakatifu, basi mimi nitawajibika kupewa kila adhabu na kustahiki kila dhila. Nasema kwa kusisitiza sana kuwa kwa kiroho maisha ya Wakristo ni machafu sana. Yule Mungu Mtukufu Aliye Mungu wa mbingu na ardhi Anachukia sana hali zao za kiitikadi kama tunavyochukia mzoga mchafu sana uliooza. Kama mimi ni mwongo katika jambo hilo, na kama katika kauli hiyo Mungu Hayupo pamoja nami, basi njooni mfanye uamuzi kwa utulivu na upole. Nasema tena kuwa ndani ya Wakristo hamna maisha matakatifu yanayoshuka kutoka mbinguni na kung’arisha mioyo. Bali kama nilivyoeleza huko nyuma, baadhi yao wanao

uungwana wa kitabia kama walivyo katika mataifa mengine. Basi sizungumzii uungwana wa asili; kwani wapole na waungwana wa aina hii hupatikana kiasi fulani katika kila kaumu hata matopasi na watengeneza ngozi hawako nje ya kanuni hii. Bali nazungumzia kuhusu maisha matakatifu ya kimbinguni yanayopatikana kutokana na Neno hai la Mungu yanayoshuka kutoka mbinguni na huwa na alama ya kimbinguni. Basi, haya hayamo ndani ya Wakristo. Sasa mtu yeyote atufahamishe kuna faida gani ya dhabihu ya kilaana?

Sasa, baada ya kwisha kutolewa maelezo ya njia ya wokovu ambayo Wakristo wanainasibisha kwa Yesu, swali linazuka kitabia kuwa je, ujumbe wa Mtume wetu s.a.w. pia ndio mapenzi hayo hayo ya kilaana, na dhabihu ya kilaana kwa utakaso na wokovu wa binadamu au kuna njia nyingine? Jibu lake ni kuwa Islam imeepukana kabisa na njia hii chafu na najisi, haifundishi dhabihu yoyote ya kilaana wala haifundishi upendo wa kilaana; bali imetufundisha kuwa ili kupata utakaso wa kweli tujitolee dhabihu takatifu ya nafsi zetu, iliyooshwa kwa maji ya ikhlasi na kutakaswa kwa moto wa ukweli na subira, kama Anavyosema:

بَلٰى ۚ مَنْ اَسْلَمَ وَجْهَهٗ لِلّٰهِ وَهُوَ مُحْسِنٌ فَلَهٗۤ اَجْرُهٗ
عِنْدَ رَبِّهٖ ۪ وَلَا خَوْفٌ عَلَيْهِمْ وَلَا هُمْ يَحْزَنُوْنَ ﴿١١٣﴾[7]

Yaani mtu ambaye anajitupa kwa Mungu na kujitoa wakfu maisha yake katika njia Zake na kujibidiisha kutenda mema, basi huyo atapata malipo yake kutoka kwa chemchem ya ukaribu wa Mola wake. Na juu ya watu hao haitakuwa hofu wala huzuni yoyote. Yaani mtu ambaye anatumia nguvu zake zote katika njia ya Mungu, na kauli yake na amali yake, kutikisika kwake na kutulia kwake, na maisha yake yote ndiyo kwa ajili ya Mungu tu, na anajitahidi daima kufanya wema wa kweli, basi mtu huyo Mungu Atampatia malipo kutoka Kwake, na Atamwokoa katika hofu na huzuni.

Ikumbukwe kuwa neno hili la Islam lililotumika hapa, kwa maneno mengine limeitwa *istikamat* (uimara) ndani ya Kurani Tukufu, kama Anavyofundisha dua hii:

اِهْدِنَا الصِّرَاطَ الْمُسْتَقِيْمَ ۙ﴿٦﴾ صِرَاطَ الَّذِيْنَ اَنْعَمْتَ عَلَيْهِمْ ۙ[8]

Yaani utuimarishe katika njia imara, njia ya wale waliopata neema kutoka kwake na waliofunguliwa milango ya kimbinguni. Ibainike ya kwamba uimara wenyewe wa kitu hufahamika kwa kuangalia kusudio hasa la kuwepo kwake. Na kusudio hasa la kuwepo

---

[7] Al-Baqara 2:113
[8] Al-Faatiha1:6-7

kwa binadamu ni kwamba binadamu ameumbwa kwa ajili ya Mungu. Basi, uimara wenyewe wa mtu ni kwamba yeye awe kwelikweli kwa Mungu jinsi alivyoumbwa kwa ajili ya utii wa kudumu. Na pindi atakapokuwa kwa ajili ya Mungu kwa nguvu zake zote, ndipo bila shaka neema itamshukia yeye ambayo kwa maneno mengine tunaweza kuita maisha matakatifu. Kama mnavyoona, dirisha la upande wa jua linapofunguliwa, miali ya jua lazima huingia ndani, vivyo hivyo mtu anapomwelekea kabisa Mwenyezi Mungu na kusiwe na pazia yoyote baina yake na Mwenyezi Mungu, ndipo mara mwako wa nuru humteremkia na kumwangaza na kumwondolea uchafu wake wote wa ndani. Ndipo yeye anakuwa mtu mpya na hutokea badiliko kubwa ndani yake, na hapo husemwa mtu huyo amepata maisha matakatifu. Mahali pa kujipatia maisha hayo matakatifu ni dunia hii hii. Kwenye habari hiyo Mungu Mtukufu Anaashiria katika aya hii:

مَنْ كَانَ فِيْ هٰذِهٖٓ اَعْمٰى فَهُوَ فِي الْاٰخِرَةِ اَعْمٰى وَاَضَلُّ سَبِيْلًا ○[9]

Yaani, mtu aliyebaki kipofu katika dunia hii, wala hakupewa nuru ya kumwona Mungu, huyo atakuwa kipofu katika akhera pia. Ilimuradi, kutoka katika dunia hii hii mtu hujichukulia hisia. Asiyepata hisia hizo katika dunia hii na imani yake iliishia kwenye

---

[9] Banii Israaiil,17: 73

visa na hadithi tu, yeye mtu huyo daima ataingia gizani. Ilimuradi, kwa kujipatia maisha matakatifu na wokovu wa kweli Mwenyezi Mungu Ametufundisha kuwa sisi tuwe kabisa wa Mungu, na tuangukie kizingiti chake kwa uaminifu wa kweli na tujiepushe kabisa na kitendo hiki kibaya cha kumwita kiumbe kuwa Mungu hata kama tukiuawa na kukatwa vipande vipande na kuchomwa katika moto, tupige muhuri kwa damu zetu juu ya imani ya kuwepo kwa Mungu. Ndiyo maana, Mungu Ameiita dini yetu jina Islam, ili iwe ishara kwamba tumeisha jitupa kwa Mungu. Na kanuni ya asili inashuhudia kwa uwazi ya kwamba njia iiyofundishwa na Kurani ya kupata utakaso na wokovu wa kweli ndiyo njia inayopatikana katika ulimwengu wa kiwiliwili pia. Tunaona kila siku kwamba kwa kupata chakula kibaya na kukosa chakula kizuri wanyama wote na mimea hupata maradhi. Na kanuni ya asili imeweka njia hii ya kuyazuia maradhi kwamba kwa kilaji vitu vifaavyo vipatikane na vibovu vizuiwe. Kwa mfano, iangalieni miti, hiyo kwa kustawi ina sifa mbili: Ya kwanza, hiyo huendelea kupenyeza mizizi yake ardhini ili isikauke ikikaa nje. Ya pili ni kwamba hiyo huvutia kwake maji ya ardhini kwa kapilari za mizizi yake na kwa njia hii inastawi. Basi, na kanuni hiyo imeweka ulimwanguni kwa binadamu. Yaani, yeye anafaulu hapo tu ambapo kwanza anajiimarisha katika Mungu kwa ikhlasi na uthabiti, na kwa kuomba

ghofira anapenyeza mizizi yake katika mapenzi ya Mungu na kisha kwa kutubu kwa kauli na amali akielekea kwa Mungu huyavutia kwake maji ya Mungu kwa kapilari za unyenyekevu. Na kwa njia hii huyavutia maji kwake namna ambavyo huyaoshelea mbali ukavu wa dhambi na kuondoa udhaifu.

Na kuomba ghofira ambako husababisha mizizi ya imani kuimarika kumetumika katika Kurani Tukufu katika maana mbili. Ya kwanza ndiyo kwa kuimarisha moyo katika mapenzi ya Mungu kuzuia dhambi zinazochemka katika hali ya faragha isitendeke kwa sababu ya uhusiano na Mwenyezi Mungu, na kutaka msaada kutoka kwa Mungu kwa kuungana naye. Kuomba huko ghofira ndiyo kwa wale waliokurubiwa na Mungu ambao wanaona kutengana na Mungu hata kwa muda wa kupepesa macho ndiyo kujiangamiza, kwa hiyo wanaomba ghofira ili Mungu Aendelee kuwabakiza katika mapenzi Yake. Na aina ya pili ya *istighfar* ndiyo kumkimbilia Mungu baada ya kuachana na dhambi, na kufanya bidii kwamba moyo uimarike katika huba ya Mungu jinsi mti uimarikavyo katika ardhi, ili uepukane na ukavu wa dhambi na uchakavu kwa kupata ustawi mwema. Hali hizo mbili zimeitwa *istighfar*, kwani *istighfar* limetokana na neno *Ghafr* linalomaanisha kufunika na kufukia. Kana kwamba maana ya *istighfar* ni kwamba Mungu Aendelee

kufukia dhambi za mtu anayejiimarisha katika mapenzi Yake na Asiiache 'mizizi' ya ubinadamu kubaki nje bali Akiifunika katika shuka ya Uungu Ampatie hisa katika Utukufu Wake, au kama mzizi wowote umekuwa wazi kwa sababu ya kutendeka dhambi, basi na Aufunike na kukinga na athari mbaya ya kuwa kwake wazi. Basi, kwa vile Mungu ni chanzo cha baraka, na nuru yake iko tayari wakati wote kuondoa kila aina ya giza, kwa hiyo njia iliyonyooka ya kupata maisha matakatifu ni kwamba kwa kuhofia hali hii ya kutisha tunyoshe mikono yetu kwenye chemchem hiyo ya utakaso, ili chemchem hiyo itusogelee kwa nguvu na kuuondolea mbali uchafu wote mara moja. Hakuna dhabihu yoyote yenye kumridhisha Mungu kuliko hii kwamba kwa kukubali kufa katika njia yake tujitupe sisi mbele yake. Hiyo dhabihu Mungu Ametufundisha kutoa, kama Anavyosema:

لَنْ تَنَالُوا الْبِرَّ حَتّٰى تُنْفِقُوْا مِمَّا تُحِبُّوْنَ ط[10]

Yaani hamwezi kuufikia wema hasa mpaka mtoe katika njia ya Mungu vitu vyote mnavyovipenda.

Hiyo ndiyo njia tuliyofundishwa na Kurani Tukufu. Na shuhuda za mbinguni zatangaza kwa sauti ya juu kuwa hiyo ndiyo njia iliyonyoka, na akili pia inatoa ushuhuda juu yake. Basi jambo ambalo limethibitika

[10] Aali'Imraan 3: 93

na mashahidi mbele yake haliwezi kuthubutu lisilokuwa na ushahidi wowote. Yesu Mnazareti akafuata mafundisho ya Kurani, ndiyo maana akapata neema kutoka kwa Mungu. Vivyo hivyo mtu yeyote atakayefuata mafundisho matakatifu hayo naye atakuwa kama Yesu. Mafundisho haya matakatifu yako tayari kuwafanya maelfu ya watu kuwa Yesu Masihi na tayari yamekwisha wafanya malaki.

Kwa upole sana na adabu tunawauliza waheshimiwa mapadri kuwa baada ya kumfanya mtu huyo maskini dhaifu kuwa Mungu mmepata maendeleo gani ya kiroho? Mkithibitishia maendeleo hayo basi tuko tayari kupokea. La sivyo, enyi wenye bahati mbaya mnaoabudu viumbe! njooni mkaone maendeleo yetu na kusilimu. Je, si jambo la uadilifu kuwa yule mtu ambaye anao ushahidi wa kimbinguni juu ya maisha yake matakatifu na utambuzi wake mtakatifu na upendo wake mtakatifu ndiye mkweli. Na yule ambaye ana visa na hadithi pekee ndiye mwenye bahati mbaya, mwongo na mla uchafu.

## Swali la pili:

Endapo shabaha ya lslam ni kuwaleta watu kwenye Umoja wa Mungu, basi ni sababu gani, mwanzoni mwa Islam vita vilipiganwa dhidi ya Mayahudi ambao vitabu vyao havifundishi chochote isipokuwa Umoja wa Mungu? Au kwa nini siku hizi Mayahudi au wengine wenye kuamini umoja wa Mungu wafikiriwe kulazimika kusilimu kwa kupata wokovu?

**Jibu:** Iwe wazi kuwa katika zama za Mtume wetu s.a.w., Mayahudi walikuwa wamekwenda mbali na miongozo ya Torati. Ingawa ni kweli kuwa vitabu vyao vilikuwa na mafundisho ya Umoja wa Mwenyezi Mungu, lakini walikuwa hawanufaiki na Umoja huo, na wakapoteza ile shabaha hasa ambayo kwayo binadamu aliumbwa na Vitabu vilishuka. Imani katika Umoja wa kweli wa Mungu humaanisha kwamba baada ya kuamini kuwepo kwa Mungu na kukubali Umoja wake mtu ashughulikie kumtii Mungu Mkamilifu na Mhisani na kutafuta ridhaa yake na kujipoteza katika mapenzi yake. Basi, Umoja huo wa Mungu haukubaki tena ndani yao. Adhma na utukufu wa Mungu ulikuwa umetoweka mioyoni mwao. Kwa midomo walikuwa wanamtaja Mungu, lakini mioyo yao ikamwabudu shetani. Wakapita kiasi katika kuiabudu dunia na kuitafuta na katika ujanja na undaganyifu. Kati yao madarweshi na

maruhubani waliabudiwa, na matendo maovu ya aibu sana yalitendeka baina yao, na kujionyesha kulizidi, ulaghai ukawa mwingi. Ni dhahiri kuwa Tauhidi siyo kutamka tu kwa midomo لَآ إِلَٰهَ إِلَّا ٱللَّٰهُ[11] ilhali mioyoni mwao mmejumuika maelfu ya masanamu. Bali mtu ambaye anaenzi kazi, hila, undanganyifu na tadbiri yake kama vile kumwenzi Mungu, au anamtegemea mtu kama Mungu Anavyopaswa kutegemewa au anajitukuza nafsi yake kama Mungu anavyopaswa kutukuzwa, basi katika hali zote hizo yeye mtu huyo ni mwabudu sanamu mbele ya Mwenyezi Mungu. Sanamu si tu zile zinazotengenezwa kwa dhahabu au fedha au shaba nyeupe au mawe na zinategemewa, bali kila kitu au kauli au kitendo kinachoheshimiwa jinsi Mungu tu Anavyotakiwa kuheshimiwa, ni sanamu machoni mwa Mwenyezi Mungu. Naam, ni kweli kuwa ndani ya Biblia hakuna ufumbuzi huo mwepesi wa ibada ya masanamu, lakini Kurani Tukufu imejaa ufumbuzi huo. Basi shabaha moja ya Mwenyezi Mungu ya kuiteremsha Kuraini Tukufu ilikuwa kuiondoa kabisa mioyoni mwa watu ibada ya masanamu ambayo ni kama ugonjwa wa kifua kikuu uliowashika. Na katika zama hizo Mayahudi walikuwa wamezama sana ndani ya ibada hiyo ya masanamu, na Torati ilikuwa haiwezi kuwaachisha, kwani ndani ya Torati hayakuwamo mafundisho hayo

[11] Hakuna apasaye kuabudiwa ila Allah.

mepesi; na pia kwa sababu ugonjwa huo uliokuwa umeenea baina ya Mayahudi wote, ulihitaji mfano wa Tauhidi takatifu ambayo ionekane hai katika mtu mmoja mkamilifu.

Ikumbukwe kuwa Tauhidi ya kweli Anayotaka Mungu tuikiri na ambayo wokovu unafungamana nayo ndiyo kumfahamu Mungu kuepukana na kila mshirika katika dhati yake hata kama ni sanamu au mwanadamu, au jua au mwezi au nafsi ya mtu mwenyewe au tadbiri yake au hila na ulaghai wake; na kutokupendekeza dhidi yake mweza yeyote, kutoamini mtoaji riziki yeyote, kutomdhania yeyote kuwa mwenye kutoa heshima na dhila, na kutopanga msaidizi yeyote wala mwenye kuauni. Na ya pili ndiyo kumpenda Yeye pekee, kumwabudu Yeye pekee, kujinyenyekeza kwake pekee, kumtumaini Yeye pekee na kumcha Yeye peke yake. Basi Tauhidi yoyote haiwezi kukamilika pasipo hali hizi tatu za pekee: ya kwanza, tauhidi kuhusu dhati, yaani kufahamu vitu vyote kama havipo mbele ya kuwepo kwake, na kuviona vyote hivyo ni vyenye kuangamia, tena hauna uhakika. Pili, Tauhidi kuhusu sifa, yaani kutokuamini sifa za kuruzuku na Uungu kupatikana katika yeyote awaye isipokuwa katika Mungu, na kuyakini kuwa wale wanaonekana kidhahiri wanaruzuku viumbe au ni wapaji, ndio mpango wa Mkono Wake. Ya tatu, Tauhidi kiupendo na kiukweli

na kiihlasi, yaani kutomshirikisha yeyote na Mwenyezi Mungu katika mapenzi na mengineyo yaliyo alama ya ibada na kujipoteza tu ndani yake. Basi, Tauhidi hii inayojumuisha sehemu zote tatu na ni msing asilia wa wokovu ndiyo ambayo Mayahudi walikuwa wameyapoteza. Ndiyo maana, maovu yao yanashuhudia wazi wazi juu ya jambo hili kuwa midomo yao inadai kumwamini Mungu lakini imani haimo moyoni, kama Kurani yenyewe inavyowashutumu Mayahudi na Manasara na inasema kuwa kama watu hao wangesimamisha Torati na Injili, wangepewa riziki za kimbinguni na za ardhini pia. Yaani miujiza ya kimbinguni na maombi kukubaliwa na kashf na funuo ambazo ni alama za waaminio zilizo riziki ya kimbinguni zingepatikana kati yao. Na riziki ya kiardhi pia ingepatikana. Lakini, sasa hao wamekosa kabisa riziki ya kimbinguni, na riziki ya kiardhi pia hawapati kwa kuelekea kwa Mungu bali kwa kuelekea dunia tu. Basi riziki zote mbili wamenyimwa.

Sasa ikumbukwe pia kwamba inathibitika bila shaka kutoka katika mafundisho ya Kurani kuwa vita vilipiganwa dhidi ya Mayahudi na Wakristo, lakini vita hivyo havikuanzishwa kamwe na Waislamu. Na vita hivyo havikuwa kuwaingiza kwa nguvu katika dini, bali vilipiganwa ambapo wapinzani wa Islam wenyewe walisababisha vita hivyo kwa kutesa au

kuwasaidia watesi. Na sababu zilipoletwa nao hao wenyewe, hapo ghera ya Mungu ikataka kuyaadhibu mataifa hayo. Hata hivyo rehema ya Mungu ikafanya huruma ya kwamba mwenye kusilimu au mwenye kutoa jizia ataepuka adhabu hiyo. Huruma hiyo nayo ilikuwa sawa na kanuni ya tabia ya asili, kwani kila balaa linaloshuka kama adhabu, kwa mfano ugonjwa wa kuambukiza au njaa, wakati huo dhamira ya watu inaelekea yenyewe kutaka adhabu iondolewe kwa maombi, toba, unyenyekevu na kwa kutoa sadaka. Ndivyo inavyotokea daima. Hapo inathibitika kuwa Mungu, Mwingi wa rehema, Mwenyewe Anafunulia mioyoni ili kusitisha adhabu, kama ambavyo kwa kupokelewa mara kadhaa dua za Nabii Musa a.s., wana wa Israeli waliondolewa adhabu. Ilimuradi, vita vya Waislamu vilikuwa ni adhabu kwa wapinzani wakorofi, ambamo njia moja ya rehema pia ilikuwa wazi. Basi, kufikiri kwamba Islam ilipigana vita kwa kueneza Tauhidi ni kudanganyika. Ikumbukwe kuwa vita vilianza kupiganwa ili kuadhibu ambapo mataifa mengine yalipopania kushindana na kudhulumu.

Ama swali hili kuwa Mayahudi walikuwa na haja gani ya kusilimu ilihali walikuwa wanamwami tayari Mungu mmoja, basi tumekwisha lijibu sasa hivi kwamba Tauhidi haikuwemo katika mioyo ya Mayahudi. Ilikuwa ndani ya vitabu tu, tena hiyo ilikuwa pungufu. Basi, ilikuwepo haja ya kujipatia

roho hai ya Tauhidi, kwani maadamu roho hai ya tauhidi haiimariki ndani ya moyo wa mtu, wokovu hauwezi kupatikana. Mayahudi walikuwa kama wafu; na kwa sababu ya ugumu wa mioyo na uasi wa aina mbalimbali roho hiyo hai ilikuwa imetoweka kutoka ndani yao. Hawakubakia na mwelekeo wowote kwa Mungu. Na Torati yao kwa sababu ya mafundisho mapungufu na kwa sababu ya kugeuzwa maneno na maelezo, ikawa haifai tena kuwa kiongozi kamili. Ndiyo maana, Mungu Akateremsha ufunuo hai mithili ya mvua mpya na kuwaita kwenye ufunuo huo ulio hai, ili wakiepuka madandaniyfu na makosa ya aina mbalimbali wapate wokovu wa kweli. Hivyo, haja moja ya kuteremka Kurani ilikuwa kuwafundisha Mayahudi waliokuwa kama wafu, tauhidi iliyo uhai; pili, ili kuwatanabahisha juu ya makosa yao ya tatu, ili kuwaelimisha yale kinaganaga juu ya masaala ambayo yamedokezwa tu katika Torati kama vile masaala ya ufufuo na masaala ya roho kubaki na masaala ya Pepo na Jahanamu.

Ni kweli kuwa mbegu ya ukweli ilipandwa na Torati, na kwa Injili mbegu hiyo ikajitokeza kama mtoa bishara kwa siku zijazo; na kama mimea ya shamba inavyoitokeza barabara, safi na mizuri kabisa, na hali yake inabashiria kwamba baadaye matunda mazuri na vichala vizuri viko tayari kujitokeza. Vivyo hivyo Injili ilikuja kutoa bishara ya ujaji wa sheria kamili na

kiongozi kamili, na mbegu hiyo ilifikia ukamilifu wake kwa ujaji wa Furkan (Kuran) ambayo ilileta pamoja nayo neema kamilifu iliyopambanua kabisa baina ya haki na batili, na ikayafikisha maarifa ya dini kwenye ukamilifu, kama ilivyoandikwa ndani ya Torati hapo awali: 'Bwana alitoka Sinai akawaondokea kutoka Seiri, aliangaza katika kilima cha Paran.'[12]

Ni jambo lililothibitika kabisa kwamba Kurani pekee ndiyo iliyoionyesha kila jiha ya sheria katika sura kamili. Sheria ina sehemu mbili kubwa: Haki ya Mungu na haki ya watu. Kurani Tukufu peke yake ndiyo iliyotimiza sehemu zote hizo mbili. Kazi ya Kurani Tukufu ilikuwa kuwafanya washenzi kuwa binadamu, na kuwafanya binadamu wawe waja wa Mungu. Na imetimiza kazi hii kwa namna ambavyo mbele yake Torati ndiyo kama bubu.

Miongoni mwa haja za Kurani, mojawapo ilikuwa kuondoa hitilafu iliyokuwa baina ya Wakristo na Mayahudi kuhusu Hadhrat Masihi a.s. Basi Kurani Tukufu ikaamulia magomvi hayo yote kama ilivyo aya hii ya Kurani Tukufu kwa kutoa uamuzi wa ugomvi huo: [13] يٰعِيْسٰٓى اِنِّىْ مُتَوَفِّيْكَ وَرَافِعُكَ اِلَىَّ...

[12] Kumbukumbu la Torati 33:2

[13] Kwa yakini mimi nitakufisha na nitakuinua kwangu. Aali‘Imraan 3:56

Kwani, Mayahudi walidhani kuwa nabii wa Wakristo, yaani Yesu Masihi, alisulubiwa, kwa hiyo sawa na mafundisho ya Torati alilaaniwa na hakurufaishwa; na hii ndiyo dalili ya kuwa kwake mwongo. Na Wakristo wakadhani kwamba kweli akalaaniwa, lakini kwa ajili yetu, na baadaye laana ikaondoka na akarufaishwa, na Mungu Akamkalisha kwenye mkono wake wa kulia. Sasa, aya hiyo ikatoa hukumu kuwa alirufaika papo hapo. Siyo kama walivyodhani Mayahudi kuwa alipata laana ya kudumu inayozuia kurufaishwa kwenye Mungu, wala siyo kama walivyodhani Wakristo kuwa laana ilibaki kwa siku chache kisha akarufaishwa kwa Mungu; bali akarufaishwa kwa Mungu papo hapo alipofariki. Na ndani ya aya hizo hizo Mwenyezi Mungu Akafahamisha pia kuwa kurufaika huku siyo kinyume cha maagizo ya Torati, kwani Torati inahukumu kutokurufaika na kupata laana pindi auawapo mtu msalabani. Lakini kwa kuguswa tu na msalaba au kupata mateso msalabani yasiyosababisha kifo hakuleti laana wala hakuzuii kurufaishwa. Kwani Torati yamaanisha kwamba Mwenyezi Mungu Ameweka msalaba kuwa njia ya kuwaua wahalifu. Basi mtu aliyefia msalabani amekufa kifo cha kihalafa kilicho kifo cha laana. Lakini Masihi hakufia msalabani, na Mungu Alimwokoa katika kifo cha msalabani. Bali kama alivyokuwa amesema kwamba hali yangu inafanana na hali ya Yona, ndivyo

ilivyotendeka. Yona hakufa tumboni mwa samaki, wala Yesu msalabani, na dua yake 'Eli eli lama sabaktani'[14] ikakubaliwa. Kama angekufa lazima balaa lingemsibu Pilato pia, kwani malaika alimwonya mke wa Pilato kuwa endapo Yesu atakufa ukumbuke nyinyi pia mtaangukiwa na balaa. Lakini Pilato hakupata balaa lolote. Na alama mojawapo ya Yesu kubaki hai ni hii pia kwamba katika tukio la msalaba mifupa yake haikuvunjwa, na baada ya kushushwa kutoka msalabani damu pia ikamtoka kwa kuchomwa (mkuki). Na akawaonyesha wanafunzi wake majeraha yake baada ya tukio la msalaba. Na ni dhahiri kuwa katika maisha mapya ilikuwa haiwezekani kuwa na majeraha. Basi, imethibitika kuwa Yesu hakufia msalabani, hivyo akawa si mlaaniwa na bila shaka alikufa kifo kitakatifu, na kama mitume wote watukufu wa Mungu, yeye pia akarufaishwa kwa Mungu baada ya kufariki. Na sawa na ahadi [15]يٰعِيْسٰٓى اِنِّىْ مُتَوَفِّيْكَ وَرَافِعُكَ اِلَيَّ akarufaishwa kwa Mungu. Kama angefia msalabani, angethibitika kuwa mwongo kwa mujibu wa kauli yake mwenyewe, kwani hapo asingefanana na Yona hata kidogo.

Basi, ugomvi huo ulikuwa uliendelea kati ya Mayahudi na Wakristo kuhusu Masihi, ambao hatimaye uliamuliwa na Kurani Tukufu. Hata hivyo

---

[14]'Mungu wangu, Mungu wangu, mbona umeniacha?' Mathayo 27:46

[15]Kwa yakini mimi nitakufisha na nitakuinua kwangu. Aali‘Imraan 3:56

Wakristo mpaka sasa wanasema kuwa kulikuwa na haja gani ya kushuka Kurani? Enyi msiojua, na vipofu wa mioyo, Kurani Tukufu imeleta tauhidi kamili; Kurani ikalinganisha akili na Maandiko; Kurani ikaifikishia tauhidi ukamilifu; Kurani imetoa hoja juu ya tauhidi na sifa za Mungu, na imethibitisha kuwepo kwa Mungu kwa hoja za kiakili na za maandiko na ikahakikisha kwa njia ya kashfi pia; na dini ambayo hapo awali ilikuwa kama visa na masimulizi, ikaihakikisha kielimu; na ikaeleza hekima ya kila itikadi; na silisila ya maarifa ya dini isiyokuwa kamili ikaifikishia ukamilifu; na ikamwondelea mbali Yesu laana, na ikatoa ushahidi juu ya kurufaishwa kwake na kuwa kwake nabii wa kweli. Basi, je, pamwe na ukarimu huo wote bado haijathibitika haja ya Kurani Tukufu?

Ikumbukwe kuwa Kurani imethibitisha kwa uwazi sana haja ya ujaji wake: Kurani inasema wazi wazi:

إِعْلَمُوٓا اَنَّ اللّٰهَ يُحْيِ الْاَرْضَ بَعْدَ مَوْتِهَا ؕ[16]

Yaani, tambueni kwamba ardhi ilikuwa imekufa, na sasa Mungu Ataihuisha upya. Historia inashuhudia kuwa karibu na zama za ushukaji wa Kurani kila taifa lilikuwa limeharibika mienendo yake. Padri Fandal mwandishi wa kitabu '*Mizanul Haq*' juu ya chuki nyingi iliyokuwa imejaa moyoni mwake anatoa

[16] Al-Hadiid 57:18

ushahidi bayana katika '*Mizanul Haq*' kuwa katika zama za ujaji wa Kurani mienendo ya Mayahudi na Wakristo ilikuwa imechafuka na hali zao zilikuwa zimeharibika sana, na ujaji wa Kurani ulikuwa onyo kwao. Lakini mjinga huyo, juu ya kukiri kuwa hali ya Mayahudi na Wakristo ilikuwa mbaya ilipokuja Kurani, akaleta udhuru wa uwongo kuwa Mungu alikusudia kuwaonya Mayahudi na Wakristo kwa kumtuma Nabii mwongo. Lakini huku ni kumsingizia Mwenyezi Mungu. Je, tunaweza kuinasibisha desturi hii chafu kwa Mwenyezi Mungu kwamba Yeye akiwakuta wamepotea na kuharibika mienendo akafikiria mpango kwamba awaletee sababu za kuwapoteza zaidi, na kuwatumbukiza mamilioni ya watu wake katika maangamio kwa mkono wake mwenyewe? Je, katika kanuni ya asili ya Mwenyezi Mungu hii ndiyo desturi yake inayothibitika wakati shida na taabu zinaposhinda. Ni sikitiko sana kuwa watu hao wakiwa na huba ya dunia wanalitemeaje jua! Wanamwita mtu mmoja mnyonge kuwa Mungu, tena mlaaniwa pia; na wanamkana Nabii mwenye shani kubwa aliyekuja wakati binadamu walipoanza kuwa kama wafu na bado wanasema kulikuwa na haja gani ya Kurani? Enyi mlioghafilika na mlio vipofu wa mioyo, jinsi ilivyokuwa tufani ya upotevu ilipokuja Kurani, hakuna nabii yeyote aliyekuja katika wakati kama huo. Iliikuta dunia kuwa kipofu ikaijaalia mwanga; iliikuta potofu ikaipa mwongozo; iliikuta

imekufa ikaihuisha. Je bado ipo kasoro yoyote katika kuthibitika haja? Na kama mkisema tauhidi ilikuwepo hata hapo kabla, Kurani imeleta kitu gani kipya, basi naisikitikia akili yenu sana. Nimeshaandika sasa hivi kuwa tauhidi ilivyoelezwa katika vitabu vya awali ilikuwa pungufu, nanyi hamwezi kuthibitisha kwamba ilikuwa kamilifu: Isitoshe, tauhidi ilikuwa imetoweka kabisa mioyoni, Kurani ikaikumbushia tauhidi hiyo tena na kuikamilisha; ndiyo maana, Kurani inaitwa Ukumbusho, kwani inakumbusha. Hebu fumbueni macho mkaone kwamba je, yote iliyoelezea Torati kuhusu tauhidi, yalikuwa ni jambo jipya wasilolijua manabii wa zamani? Je, si kweli kuwa kwanza kabisa Adamu, kisha Shithi[17] na Nuhu na Ibrahim na manabii wengine waliokuja kabla ya Musa walifundishwa tauhidi? Basi hata Torati inapata lawama hii kwamba imeleta kitu gani kipya? Enyi watu wenye mioyo iliyopinda, Mungu Hawezi kuwa mpya kila siku. Aliyekuwa Mungu katika zama za Musa ndiye Aliyekuwa katika zama za Adamu, Shithi, Nuhu, Ibrahimu, Isihaka, Yakobo, na Yusufu. Na Torati ikaeleza kuhusu tauhidi yale yale waliyoendelea kueleza Manabii waliopita.

Sasa, kama iulizwe kwa nini Torati ilitaja tauhidi ile ile ya zamani, basi jibu lake ni kuwa habari ya kuwepo kwa Mungu na Umoja wake haikuanzia na

[17] Shithi alikuwa Nabii. Yeye alikuwa mtoto wa Nabii Adamu a.s.

Torati bali inaendelea kujulikana tangu kale. Naam, katika baadhi za zama, kwa sababu ya kuachwa matendo bila shaka iliendelea kuhakirika na kudhalilika machoni mwa watu wengi. Basi, jukumu la Vitabu vya Mungu na Manabii wa Mungu lilikuwa kwamba waliendelea kutokea katika zama ambapo watu walipungukiwa maelekeo kwenye masaala ya tauhidi na wakaangukia ushirikina wa aina mbalimbali. Masaala hiyo ilikatulika mara elfu kadha duniani, na tena mara elfu kadha ikishika kutu ikafichikana machoni mwa watu. Na ilipofichikana, Mungu Akamtuma mja wake ili aionyeshe kwa kuing’arisha upya. Hivyo ndivyo ilivyoendelea kushinda duniani pengine giza na pengine nuru; na hiki ni kipimo cha daraja la juu kabisa la kumtambua kila nabii kwamba iangaliwe alikuja wakati gani na akapata kurekebisha kiasi gani. Yafaa wafikirie tu jambo hili kwa kutafuta ukweli wala wasijali kauli za kudanganya za wakorofi na wenye chuki, na kwa nia safi wachunguze hali za nabii yeyote kwamba alipodhihiri aliwakuta watu wa zama zile katika hali gani, na kisha akawaletea mabadiliko gani katika itikadi na mienendo ya watu hao. Hapo lazima itajulikana kwamba nabii gani alikuja ilipokuwa haja kali sana na yupi ilipokuwa haja kiasi. Nabii anahitajika kwa wenye dhambi kama ahitajikavyo tabibu kwa wagonjwa. Na kama wingi wa wagonjwa

unavyomhitaji tabibu, vivyo hivyo wingi wa wenye dhambi unavyomhitaji mrekebishaji.

Sasa kama mtu akiizingatia kanuni hii atalii historia ya Uarabuni kwamba Waarabu walikuwa na hali gani kabla ya kudhihiri Mtume Mtukufu s.a.w. na kisha wakawaje, hapo bila shaka atamtambua huyu Nabii wa zama za mwisho s.a.w. kuwa mwenye daraja la kwanza baina ya manabii wote katika nguvu takatifu na athari imara na kutoa baraka, na kwa sababu hiyo yeye atakuwa na yakini isiyokanika ya haja ya ujaji wa Mtume Mtukufu s.a.w. na Kurani kuliko haja ya vitabu vingine vyote na manabii wote. Kwa mfano, Yesu akija duniani alikidhi haja gani ya dunia? Na kuna uthibitisho gani kwamba alikidhi haja yoyote? Je, akaleta badiliko kubwa ndani ya hulka, mazoea na imani ya Mayahudi? Au aliwafikishia wanafunzi wake ukamilifu katika utakaso wa nafsi? Bali, haithibitiki kitu kati ya marekibisho hayo matakatifu. Na kinachothibitika ni hiki tu kwamba watu wachache wenye tamaa na uchu wakaungana naye; nao hatimaye wakiwa wakavu wa macho wakaonyesha si waaminifu. Kama Yesu alijiua, hapo sitakubali zaidi ya hii kwamba akapata kutenda jambo la kijinga lililomtilia kwa kudumu dosari uanadamu wake na akili yake. Tendo ambalo sheria za kibinadamu pia zinalihesabu miongoni mwa jinai, je hilo linaweza kutendeka na mtu yeyote mwenye akili

timamu. Hapana asilani! Basi, twauliza Yesu alifundisha nini na alitoa nini? Je, dhabihu ile ya kilaana ambayo sawa na akili na uadilifu hayajulikani matokeo yake yoyote.

Ikumbukwe kuwa katika mafundisho ya Injili hakuna ubora wowote mpya, bali mafundisho hayo yote yamo ndani ya Torati na sehemu yake kubwa mpaka sasa bado imo katika *Talmud*, kitabu cha Mayahudi. Na wanachuoni wa Mayahudi mpaka sasa wanalalamika kuwa mistari fulani fulani imeibiwa kutoka ndani ya vitabu vyao vitakatifu. Hivi karibuni kitabu cha mtaalamu mmoja wa Kiyahudi nilicholetewa, yeye ameandika kurasa kadhaa kwa kuthibitisha jambo hilo hilo na akatoa marejeo kwa kusisitiza kuwa mafungu fulani ya maneno yameibiwa kutoka sehemu fulani na fulani. Niliviagiza vitabu hivyo hasa kwa ajili ya Mian Sirajuddin, lakini bahati yake mbaya akaondoka kabla hajaviona. Wakristo watafiti wanakubali kwamba kwa kweli Injili ni muhtasari wa mafundisho ya vitabu vya Mayahudi yaliyompendeza Hadhrat Masihi a.s, lakini hatimaye wanasema kuwa shabaha ya ujaji wa Masihi duniani haikuwa kuleta mafundisho yoyote mapya, bali utashi hasa ulikuwa kujitolea dhabihu, yaani dhabihu hiyo hiyo ya kilaana ambayo nataka nisiitaje katika kijitabu hiki mara kwa mara. Ilimuradi, Wakristo wamedanganyika kuwa

sheria imekwisha kamilika mpaka Torati, kwa hiyo, Yesu hakuleta sheria yoyote, bali akaja akileta njia za wokovu; na eti Kurani ikaweka tena bila sababu msingi wa sheria iliyokwisha kamilika tayari. Udanganyifu huo ndio uliowaharibia Wakristo imani yao. Lakini ikumbukwe kuwa jambo hili siyo sahihi kabisa, bali ukweli hasa ni huu kuwa kwa vile binadamu ameumbwa akiwa ana tabia ya kusahau-sahau, na amri za Mungu haziwezi kudumu baina ya binaadamu kwa kitendo, kwa hiyo daima anahitajika mkumbushaji mpya na mwenye kutilia nguvu. Lakini Kurani Tukufu haikushuka kwa sababu ya haja hizo mbili tu, bali hiyo kwa kweli inatimiliza na kukamilisha mafundisho ya awali. Kwa mfano, Torati imetilia makazo sana kulipilza kisasi sawa na hali ilivyokuwa, na Injili kulingana na hali na mazingira yalivyokuwa imekazania kusamehe, kuonyesha subira na kuachilia mbali kukosewa. Na Kurani katika hali hizo mbili inafundisha kuchukua hatua sawa na hali ilivyo. Vivyo hivyo Torati imeenda upande wa kuzidisha katika kila jambo na Injili upande wa kupunguza. Lakini Kurani Tukufu inatoa mafundisho ya wastani, na inafundisha kuzingatia hali na mazingira. Ingawa mafundisho yenyewe ya vitatu vyote vitabu ni mamoja tu, lakini kimoja kimeelezea upande fulani kwa kukazania sana na kingine upande mwingine, na kingine tena kwa kuzingatia tabia ya asili ya binadamu kimeshikilia njia ya katikati

ambayo ndiyo njia ya Kurani kufundisha. Na kwa kuwa kuzingatia hali na mambo yalivyo ndiyo hekima, hivyo Kurani Tukufu tu ndiyo iliyofundisha hekima hiyo. Torati inavutia kwenye ukali usio na maana[18] na Injili inatilia mkazo msamaha usiofaa, na Kurani Tukufu inakazania kuzingatia hali na mazingira yalivyo. Basi, kama ambavyo damu ikiingia titini hugeuka kuwa maziwa, ndivyo ambavyo mafundisho ya Torati na Injili yakiisha ingia ndani ya Kurani yakawa hekima. Kama Kurani Tukufu isingekuja, Torati na Injili zingekuwa kama mshale wa kipofu unaoipata shabaha pengine mara moja tu lakini unaikosa mara mia. Ilimuradi, sheria ikaja kama visa kutokana na Torati na ikadhihirika kama mifano kutoka katika Injili, na kutoka katika Kurani Tukufu watafutao haki na uhakika wakaipata kwa sura ya hekima.

Basi Torati na Injili zitashindanaje na Kurani? Kama wakitaka kulinganisha hizo na sura ya kwanza tu ya Kurani Tukufu, yaani Sura Al-Faatiha iliyo na aya saba pekee ambayo ndani ya sura hiyo mna mamia ya kweli na maarifa za kidini na hekima za kiroho kwa utaratibu ufaao sana na utungo imara na nidhamu ya asili, juhudi zao hazitafua dafu hata kama wajaribu

---

[18] Ukali na upole huo ulifaa kulingana na hali ilivyokuwa ya zama na watu wa nyakati hizo, lakini hayakuwa mafundisho sahihi yasiyoweza kutupiliwa mbali. *Mwandishi.*

maisha mazima kuzitoa hizo kutoka katika kitabu cha Musa au kurasa chache za Injili ya Yesu. Hayo siyo majisifu, bali ni jambo la kweli na la hakika kuwa Torati na Injili hazina uwezo wa kushindana na elimu zenye hekima za Sura Al-Faatiha. Tufanyeje, na iamuliweje. Mapadri hawakubali shauri letu lolote. Kama wanaifikiria Torati au Injili yao kuwa kamilifu katika kueleza maarifa na kweli na kufafanua sifa za Neno la Mungu, tuko tayari kuwapa zawadi ya rupia mia tano taslimu, kama wakiweza kuonyesha kutoka katika vitabu vyao vyote vikubwa, ambavyo vitakuwa karibu sabini, kweli zile na maarifa za sheria na lulu za hekima zilizopangwa na johari za maarifa na sifa za Neno la Mungu tutakazoonyesha kutoka katika Sura Al-Faatiha. Kama pesa hizi ni kidogo tutaongeza kadri tuwezavyo wakileta maombi. Na kwa uamuzi safi, tutaandika kwanza maelezo ya Sura Al-Faatiha na kuyachapisha, na humo tutaeleza kinaganaga kweli zote zile na elimu za ndani, sifa za Neno la Mungu zilizomo katika Sura Al-Faatiha, na mabwana Mapadri kwa kuikabili Sura Al-Faatiha watakuwa na jukumu la kutoa kutoka katika Torati na Injili na vitabu vyao vyote kweli zile na elimu za ndani na sifa za Neno la Mungu zinazomaanisha maajabu yasiyo ya kawaida yasiyoweza kupatikana katika maneno ya binadamu. Na kama waje kushindana hivyo na waamuzi watatu kutokana na watu wa dini nyingine waseme kwamba elimu za kina na za ndani na sifa za

Neno la Mungu zilizothibitika ndani ya Sura Al-Faatiha, hizo zinathibitika pia katika ibara walizotoa hao, hapo tutawapatia rupia mia tano zitakazokuwa zimewekwa tayari pale waridhikapo.

Sasa, je, yupo padri yeyote mwenye kupiga moyo konde kushindana hivyo? Neno la Mungu linathibitika kutokana na nguvu za Mungu, kama vile sanaa zake zithibitikavyo kwa maajabu ya kudra yake. Kwa mfano, kule mbinguni kuna maelfu ya nyota, sasa kama mpumbavu fulani akiashiria kwenye nyota chache aseme hizi zina haja gani, basi hazikuumbwa na Mungu, au akitaja mimea michache au mawe au wanyama wachache aseme kuwa bila kuwepo vitu hivi mimea mingine yaweza kukidhi haja zetu, kwa hiyo hivyo havikutoka kutoka kwa Mwenyezi Mungu, basi msemaji huyo si mwingine ila mwendawazimu au mpumbavu.

Yafaa ikumbukwe kuwa Kurani imejikusanyia mafundisho yote kwa ukamilifu anayohitaji mwanadamu kwa kukamilisha nafsi yake. Na mfano wa Torati kulingana na Kurani ni kana kwamba kulikuwa na nyumba ya kupokea wasafiri ambayo ilianguka kutokana na tufani nyingi na matetemeko, ikawa rundo la matofali badala ya nyumba hiyo ya wageni. Matofali ya msalani yakaanguka jikoni na matofali ya jikoni kule msalani na nyumba nzima ikawa chini juu. Basi Mwenye nyumba hiyo ya

wasafiri akawa na huruma kwa wasafiri na badala ya nyumba hiyo ya wasafiri akajenga haraka sana nyumba nyingine ya wasafiri bora kabisa kuliko ile ya kwanza na humo mlikuwa na makazi ya kustarehesha yakipangwa kwa mpango bora na hakukupungukiwa makazi yoyote yawezayo kuhitajika. Na mwenye nyumba alipoijenga nyumba hii ya pili ya Wasafiri akatumia baadhi ya matofali ya nyumba ile ya kwanza na akaleta matofali mengine mengi na mbao na vifaa vingine vilivyoweza kutosha kalijenga jengo hili. Basi Kurani Tukufu ndiyo nyumba hii ya pili ya Wasafiri. Mwenye macho na aone.

Hapa pana shutuma inayotakiwa iondolewe kwamba kwa kuwa mafundisho ya kweli na kamili ndiyo yale ambamo izingatiwe hali ilivyo, na ielezwe kwa ukamilifu kila jambo la maarifa, basi kwa sababu gani Torati na Injili zote mbili hazina sifa hizo, lakini Kurani imezifikisha sifa hizo mbili kwenye ukamilifu. Basi jibu lake ni hili tu kuwa hiyo siyo kasoro ya Torati na Injili, bali ndio upungufu wa uwezo wa mataifa hayo. Mayahudi aliowakabili kwanza Hadhrat Musa a.s., walikaa utumwani mwa Firauni kwa miaka mia nne, na wakikaa matesoni kwa muda mrefu walisahau kabisa hakika ya uadilifu. Na ni kanuni ya asili kwamba kama mfalme ambaye huwa kama mwadabishaji na mfunzi, akiwa mwadilifu, hapo moyo wa raia pia unapata athari ya

uadilifu, na kitabia wanaelekea kwenye sifa ya uadilifu; na ustaarabu na upole ukizalika ndani yao sifa za uadilifu zinadhihirika kwa wazi. Lakini endapo mfalme ni mdhalimu, raia pia hujifunza dhuluma na ukatili na wengi wao wanakosa sifa ya uadilifu. Basi ndiyo ilikuwa hali ya wana wa Israili ya kwamba kwa sababu ya kuwa raia wa mfalme nduli kama Firauni kwa muda mrefu na kwa kuvumilia dhuluma za namna namna wakasahau kabisa kaifa ya uadilifu. Hivyo, wajibu wa Musa ulikuwa huu kwamba kwanza kabisa awafundishe uadilifu. Ndiyo maana ndani ya Torati mna aya za kuhifadhi uadilifu kwa mkazo sana. Naam, aya juu ya kuhurumia pia zaonekana ndani ya Torati, lakini kwa kuzingatia kwa makini itaonekana aya za namna hii pia zimeelezwa kwa kulinda mipaka ya uadilifu na kuzuia jazba zisizo halali na chuki isiyotakikana. Na kila mahali lengo lenyewe ni kutunza kanuni za uadilifu. Lakini kwa kusoma Injili shabaha hiyo haionekani. Bali katika Injili imesisitizwa sana kusamehe na kutokulipiza kisasi. Na tusomapo Injili kwa makini na kwa uangalifu sana, yadhihirika wazi kutokana na mfululizo wa ibara zake kwamba mwandishi wa kitabu hicho anayakini kuhusu wasomaji wake kwamba ndio watu wasio na upole kabisa wala subira wala hawako tayari kuacha kisasi, naye anataka mioyo yao igeuke hata kwamba isiwe na tamaa ya kulipiza kisasi na washike tabia ya kuonyesha subira,

kuvumilia na kusamehe. Sababu yake ndiyo tu kwamba katika zama za Hadhrat Isa a.s. hali ya khulka ya Mayahudi ilikuwa imechafuka sana; wakafikia mwisho katika kushtakiana na inadi. Na kwa kisingizio cha kuhami kanuni ya uadilifu, wakaondokewa kabisa sifa za rehema na kusamehe. Basi nasaha za Injili wakatolewa zikiwa kama kanuni iliyohusikana na zama maalum ama kanuni iliyolihusu taifa mahususi, lakini hiyo hakikuwa sura hasa ya kanuni, hivyo ikaja Kurani na kuiondolea mbali.

Tuiangaliapo Kurani Tukufu kwa makini, na tufikiapo kina cha hoja yake kwa moyo safi, yabainika wazi kwamba Kurani haikutilia makazo kulipiza kisasi wala ukali kama Torati, kama ithibitikavyo kutokana na vita vya Torati na kanuni yake ya kisasi, wala kama Injili haikuangukia mara moja mafundisho ya kusamehe na kuonyesha subira na kughofiri; bali mara kwa mara yaamrisha kutenda mema na yakataza maovu, yaani inaamrisha kwamba fanyeni lile lililo bora na sawa na hali kwa kulingana na akili na sheria, na lile lililo kinyume cha akili na sheria nalo ndilo miongoni mwa maovu liachilieni mbali. Basi kwa kusoma Kurani inaonekana kwamba Kurani yataka kuimarisha mioyoni mwetu kanuni na mipaka na maamrisho kwa njia ya kielimu, kwani hiyo haitaki kutufunga katika jela ya maamrisho na

makatazo yake yahusikanayo na watu maalumu, bali huelezea sheria yake tukufu kama kaida. Kwa mfano, inaeleza kama kaida kuwa tendeni mema na mjiepushe na maovu. Basi, maneno haya mawili, 'mema' na 'maovu', ni maneno makamilifu yanayozipa kanuni za sheria sura ya kielimu, na kulingana na mafundisho haya hakuna budi kufikiria katika kila hali kuwa wema wa kweli ni nini? Kwa mfano, sasa hivi Zaid ametukosea, basi je kumpiga ni bora au kumsamehe? Na mtu anayetuomba, kwa mfano, rupia elfu moja kwa shabaha kwamba kwa pesa hizo kijana wake aolee mke kwa shangwe na afanye sherehe hii kwa wonyesho wa kazi ya fataki na baruti, wanawake waimbaji na kwa ngoma nyingine, sawa na mila za ukoo wake. Ingawa tuna uwezo wa kumpa rupia elfu moja, lakini tunapaswa kufikiria sawa na kaida ya kuamrisha mema na kukataza maovu kwamba kwa ukarimu huo tunamsaidia mtu gani. Ilimuradi, Kurani imetuwekea sharti ya kuzingatia hali ilivyo wakati wa kutenda kila jambo jema kwa ajili ya ustawi wa dini na dunia yetu.

Basi nimeshalijibu kikamilifu swali la pili la Mian Sirajuddin na nimekwisha andika kuwa Islam haikupigana vita na Mayahudi kwa kuwalazimisha waukubali Umoja wa Mungu, bali wapinzani wa Islam wenyewe wakachochea vita kwa ukorofi wao. Baadhi yao walitangulia kuinua upanga kuwauwa

Waislamu, wengine wakawasaidia; baadhi yao walizuia bila sababu mahubiri ya Islam. Basi kwa sababu hizo zote Mwenyezi Mungu Akatoa amri ya kupingana vita dhidi ya wafisadi hao kwa kuwaponda kichwa wafisadi na kuwaadhibu na kwa kuondolea mbali shari. Na kusema kwamba kwa miaka kumi na mitatu Mtume Mtukufu s.a.w. hakupigana na wapinzani kwa sababu mpaka wakati huo alikuwa hajapata kundi la watu wengi, ni fikara ya kijeuri na ufisadi. Kama ingekuwa hivi kuwa kwa kipindi cha miaka kumi na mitatu wapinzani wa Mtume s.a.w. wangelijizuia kudhulumu na kumwaga damu walivyomwaga kule Makka, kisha wenyewe wasingelifanya njema kumwua Mtume Mtukufu s.a.w. ama kumfukuzilia mbali nchini, na Mtume s.a.w. mwenyewe bila kushambuliwa na wapinzani angelihamia Madina, hapo ingelikuwa nafasi ya kudhania vibaya hivyo. Lakini hata wapinzani wetu wanajua habari hii kwamba katika muda wa miaka kumi na mitatu Mtume wetu s.a.w. aliendelea kuvumilia kila taabu aliyopewa na maadui, na Masahaba wakaagizwa kwa kukazania wasishindane na maovu. Basi, wapinzani wakamwaga damu nyingi na kuwadhurubu Waislamu maskini, na kuwajeruhi vibaya pasipo kuhesabika. Hatimaye wakaja kuvamia ili kumwua Mtume s.a.w. Basi, katika wakati wa uvamizi huo Mungu Akamlinda Mtume wake katika shari ya maadui na kumfikisha Madina, na akampa

habari njema kuwa walioinua upanga watauawa kwa upanga tu. Hebu, pimeni kwa kutumia akili na uadilifu kwamba je maelezo hayo yaweza kumaanisha kwamba Mtume Mtukufu s.a.w. alipopata tu jamii kidogo ndipo kukaibuka nia ya vita iliyokuwa imefichika moyoni hapo kabla? Ni masikitiko tena masikitiko sana kuwa uhasama wa kidini umewafikishia hali gani wenye kuhami dini ya Kikristo! Hata hawafikiri kuwa baada ya kufika Madina watu wa Makka walipokuja kuwasaka na vita ya Badri ikapiganwa iliyokuwa vita ya kwanza ya Kiislam, jamii gani ikapata kuzuka! Wakati huo Waislamu walikuwa 313 tu kwa jumla ambao wengi wao walikuwa vijana wabichi wasio na ujuzi wa vita, waliohudhuria katika medani ya Badri. Ni jambo la kufikiria, basi, kwamba je, kwa kuwategemea watu wachache hivyo akili yaweza kuruhusu kujitokeza uwanjani kupigana na mashujaa wote wa Uarabuni na Mayahudi na Wakristo na malaki ya watu. Hapo panabainika kabisa kwamba kujitokeza huko uwanjani hakukukuwa kwa sababu ya mipango na nia zile anazofikiria mtu kuwahilikisha maadui na kujipatia ushindi. Kwani, kama ingelikuwa hivyo, ingelikuwa hakuna budi kujikusanyia kwa uchache wanajeshi elfu thelathini au arobaini, kisha baadaye kupigana na malaki ya watu.  Basi ni dhahiri kabisa kuwa vita hivyo vilipiganwa wakati wa

kulazimishwa, kwa amri ya Mwenyezi Mungu, wala siyo kwa kuzitegemea zana za kidhahiri za vita.

Hapa hakuna budi kuondoa upinzani mwingine pia, nao ni huu kuwa kama wokovu unategemea tauhidi na matendo mema yanayotendwa kwa upendo wa Mungu na hofu yake, basi kwa nini Mayahudi waliitwa kwenye Uislamu? Je, hakukubaki miongoni mwa Mayahudi hata mtu mmoja aliyeshikamana na tauhidi kwa vitendo na kuwa mtiifu mbele ya Mungu kweli kweli? Jibu lake ni kwamba tumekwisha thibitisha kuwa katika zama za ujaji wa Mtume s.a.w. Mayahudi na Wakristo wengi walikuwa waasi kama Kurani Tukufu inavyotoa ushahidi wazi wazi kuwa

وَأَكْثَرُهُمْ فٰسِقُوْنَ ○[19]

Basi, kama watu wengi miongoni mwao walikuwa waasi waliokwisha ziacha adabu za tauhidi kivitendo na matendo mema, kwa hiyo rehema ya Mungu sawa na suna yake ya zamani ikataka kuwaletea Mtume kwa kuwarekibisha. Hata tukichukulia kwamba alikuwepo baina yao mtu kwa nadra aliyekuwa mwema na mwenye imani katika taudhidi basi huyo naye hakubaki mwema kwa sababu ya kumwasi Mtume wa Mungu. Na ikiwa dhambi ndogo sana pia huchafua moyo wa mtu, basi tukubalije kwamba

[19] Yaani 'Na wengi wao ni waasi.' At-Tauba 9:8

mwasi wa Mtume wa Mungu na adui wake anaweza kubaki mwenye moyo safi?

## Swali la tatu

Katika Kurani zimo aya gani juu ya kumpenda Mungu na kumpenda mwanadamu, na Mungu kumpenda mwanadamu, ambamo hususan kitenzi cha Upendo na Huba kimetumika?

**Jibu:** Ibainike kuwa shabaha hasa ya mafundisho ya Kurani ni kwamba Mungu jinsi Alivyo Mmoja Asiye na mshirika, ndivyo ambavyo Yeye Awe wa pekee pasipo mshirika katika kupenda kwenu, kama inavyoashiria kwayo *kalima:* لَآاِلٰهَ اِلَّا اللّٰهُ

Ambayo Waislamu huikariri kila wakati. Kwani *Ilah* imetokana na *Walahu,* maana yake ni mpendwa sana anayeabudiwa. *Kalima* hii Torati haikuifundisha wala Injili; Kurani tu ndiyo iliyofundisha. Na *Kalima* hii inahusikana na Islam kana kwamba ni nishani ya Islam. Kalima hiyo hutamkwa kwa sauti kubwa kutoka minara ya misikiti wanayoichukia Wakristo na Mabaniani wote — jambo linaloonesha kuwa kumkumbuka Mungu kwa mapenzi labda ni dhambi kwao. Hii ndiyo sifa ya Uislam pekee kuwa panapokucha tu mwadhini wa Kiislam hupaza sauti akisema: اَشْهَدُ اَنْ لَّآ اِلٰهَ اِلَّا اللّٰهُ

Yaani, nashuhudia kwamba hatuna mpendwa na mwabudiwa yeyote isipokuwa Allah. Kisha wakati wa adhuhuri, sauti hiyo hiyo husikika kutoka katika

misikiti ya Kiislam; tena wakati wa alasiri na wakati wa Magharibi na wakati wa Isha pia sauti hiyo hiyo husikika na kusambaa angani. Je, mandhari hiyo huonekana katika dini nyingine yoyote duniani?

Isitoshe, hata muradi wa neno 'Islam' pia unaashiria kwenye upendo, kwani kuweka kichwa mbele ya Mwenyezi Mungu na kujiweka tayari kujitoa dhabihu ambako ndiko muradi wa Islam; hii ndiyo hali ya kimatendo iibukayo kutoka ndani ya chemchemi ya hii upendo. Yafahamika pia kutokana na neno Islam kuwa Kurani haikuufanya upendo uishie mpaka kwenye matamshi tu, bali imefundisha pia njia ya kupenda kimatendo na kujitolea uhai. Kuna dini gani nyingine duniani iliyopewa jina Islam na mwanzilishi wake? Islam ni neno la kupendeza sana, na maana za ukweli, ikhlasi na huba zimejazana ndani yake. Basi imebarikiwa dini ile inayoitwa jina Islam. Kadhalika kuhusu kumpenda Mungu Anasema Mungu Mwenye Enzi: وَالَّذِيْنَ اٰمَنُوْٓا اَشَدُّ حُبًّا لِّلّٰهِ ۭ[20]

Yaani, waaminio ni wale ambao wanampenda Mungu zaidi kuliko wote. Kisha katika sehemu nyingine Anasema: فَاذْكُرُوا اللّٰهَ كَذِكْرِكُمْ اٰبَاۗءَكُمْ اَوْ اَشَدَّ ذِكْرًا ۭ[21]

[20] Al-Baqara 2:166
[21] Al-Baqara 2:201

Yaani, Mkumbukeni Mungu kama mlivyokuwa mnawakumbuka baba zenu, bali kwa mapenzi mengi zaidi ya hayo na ya hali ya juu mkumbukeni.

Na mahali pengine Amesema tena:

قُلْ اِنَّ صَلَاتِيْ وَنُسُكِيْ وَمَحْيَايَ وَمَمَاتِيْ لِلّٰهِ رَبِّ الْعٰلَمِيْنَ ۝[22]

Yaani, uwaambie wanaotaka kukufuata kwamba hakika sala yangu na sadaka yangu, na kufa kwangu na uzima wangu ni kwa ajili ya Mwenyezi Mungu. Yaani, yule anayetaka kunifuata yeye naye atoe dhabihu hiyo. Na tena mahali pengine Akasema kuwa kama mnaona kuwa uhai wenu na rafiki zenu na bustani zenu na biashara zenu ni vipenzi zaidi kwenu kuliko Mungu na Mtume wake s.a.w. basi jitengeni nami mpaka Mwenyezi Mungu atakapotoa uamuzi. Na kadhalika Akasema mahali pengine:

وَيُطْعِمُوْنَ الطَّعَامَ عَلٰى حُبِّهٖ مِسْكِيْنًا وَّيَتِيْمًا وَّاَسِيْرًا ۝
اِنَّمَا نُطْعِمُكُمْ لِوَجْهِ اللّٰهِ لَا نُرِيْدُ مِنْكُمْ جَزَآءً وَّلَا شُكُوْرًا ۝[23]

Yaani, waaminio ni wale ambao huwalisha maskini na mayatima na wafungwa kwa sababu ya upendo wa Mungu. Na huwaambia kwamba tunawapeni kwa ajili ya huba ya Mungu na kwa radhi yake; hatutaki kwenu malipo yoyote wala hatutaki mtutolee shukrani.

[22] Al-An‘aam 6:163

[23] Ad-Dahr 76:9-10

Ilimuradi, Kurani Tukufu imejaa aya zinazosema kwamba kwa kauli na vitendo vyenu onyesheni mapenzi ya Mungu, na mpendeni Mungu zaidi kuliko chochote kiwacho. Lakini ipo sehemu ya pili ya swali hili kuwa ndani ya Kurani Tukufu wapi imeandikwa kuwa Mungu pia anawapenda watu? Basi, ibainike kuwa ndani ya Kurani Tukufu zimo aya nyingi sana zinazosema kuwa Mungu Huwapenda wanaotubu;[24] na Mungu Huwapenda watendao wema, na Huwapenda wanaofanya subira. Naam, ndani ya Kurani Tukufu hakuna palipoandikwa kuwa yule anayependa ukafiri, uasherati na dhuluma, Mungu Anampenda huyo pia. Bali katika sehemu hiyo Ametumia neno hisani, kama Anavyosema:

وَمَآ اَرۡسَلۡنٰكَ اِلَّا رَحۡمَةً لِّلۡعٰلَمِيۡنَ ○[25]

Yaani, kwa kuwahurumia walimwengu wote tumekutuma wewe. Na katika walimwengu wamo makafiri, wasio na imani, mafasiki na waovu pia. Na Amewafungulia mlango wa rehema kwa njia hii kwamba wanaweza kupata wokovu kwa kufuata miongozo ya Kurani Tukufu. Mimi nakiri kuwa ndani ya Kurani Tukufu haikuelezwa aina hii ya mapenzi ya Mungu kwa wanadamu kwamba akamsulubisha

---

[24]Anavyopenda Mungu si kama apendavyo mwanadamu ambamo kutengana huumiza na kusumbua. Bali muradi wa Mungu kupenda ni kuwa Anawatendea watendao mema kama atendavyo mwenye huba. *Mwandishi*

[25] Al-Anbiyaa 21:108

mwanaye mmoja kwa kufidia dhambi za waovu na kumtupia mwanaye mpendwa laana yao. Laana juu ya mwana wa Mungu, Mungu Atupishe mbali, ni laana juu ya Mungu Mwenyewe, kwani baba na mwana sio wawili. Na ni dhahiri kuwa laana na Uungu haviwezi kuwa pamoja. Tena fikirini pia, ni upendo gani huu alioonyeha Mungu kwa waovu wa duniani kwamba kamwua mtu mwema na kumpenda Mwovu. Hiyo ni hulka asiyoweza kuifuata mtu mnyofu.

Na sehemu ya tatu ya swali hili ndiyo kwamba ni wapi ilipoandikwa ndani ya Kurani kuwa mtu ampende mtu? Jibu lake ni kuwa katika sehemu hiyo Kurani imetumia neno 'rehema' na 'huruma' badala ya 'huba'. Maana, kilele cha huba ni ibada, kwa hiyo neno la huba kwa kweli linahusikana na Mungu.26 Katika neno la Mungu, neno la rehema na hisan limetumika kwa ajili ya wanadamu badala ya 'huba'. Kwani matokeo ya kupenda kikamilifu ndiyo kuabudu na matokeo ya kurehemu kikamilifu ndiyo kuhurumia. Watu wa mataifa mengine hawakuitambua tofauti hii, na wakawapa wengine haki ya Mungu. Siyakini kwamba Yesu aliwahi kutamka neno la ushirikina la aina hii. Bali nafikiri

[26] Neno 'kupendana' hata kama limetumika popote kwa wanadamu, halimaanishi kwa hakika huba ya kweli bali sawa na mafundisho ya Kiislamu huba ya kweli ni mahususi kwa Mungu pekee. Na huba nyinginezo si za kweli, ni za majazi. Mwandishi.

kuwa maneno hayo yachukizayo yaliingizwa baadaye ndani ya Injili, na Yesu akaaibishwa pasipo haki. Ilimuradi, katika Neno Takatifu la Mungu neno rehema limetumika kwa ajili ya wanadamu, kama anavyosema: تَوَاصَوْا بِالْحَقِّ[27] وَتَوَاصَوْا بِالْمَرْحَمَةِ[28] Yaani, waaminio ni wale ambao wanausiana kushika haki na kuhurumiana.

Na mahali pengine Anasema:

إِنَّ اللّٰهَ يَأْمُرُ بِالْعَدْلِ وَالْإِحْسَانِ وَإِيْتَآئِ ذِي الْقُرْبٰى[29]

Yaani, amri ya Mungu ndiyo kwamba wafanyieni uadilifu watu wote kwa jumla, na kwa kusonga mbele fanyeni hisani, na daraja la juu zaidi ni kwamba mwahurumie wanadamu kama jamaa wa karibu amhurumiavyo jamaa wa karibu.

Sasa inapaswa kufikiri kwamba mafudisho gani tena yatakuwa bora zaidi duniani kuliko haya ambamo kuwatendea wema wanadamu wote hakukufanywa kuishia mpaka kwa hisani tu, bali daraja la jazba ya asili pia likaelezwa linaloitwa Kuwapa ndugu.

Maana, mfanya hisani ingawa anatenda wema afanyapo hisani, lakini anataka malipo, ndiyo maana pengine humkasirikia asiye na shukureni kwa hisani

[27] Al-‘Asr 103:4
[28] Al-Balad 90: 18
[29] Al-Nahl 16: 91

aliyofanyiwa, na pengine kwa hamaki amkumbusha pia hisani yake. Lakini kufanya wema kwa jazba ya asili ambako Kurani imefananisha na wema waufanyao jamaa wa karibu, hiyo kwa kweli ni daraja ya mwisho ya wema ambayo hakuna tena daraja nyingine ya wema. Kwani, wema wa mama kwa mtoto wake na rehema yake ndiyo jazba ya asilli, na haitakikani shukrani yoyote kutoka kwa mtoto mchanga asiyejiweza.

Daraja hizo tatu ni za kuwatolea haki wanadamu zilizoelezwa na Kurani Tukufu. Sasa, tunapozisoma Torati na Injili tunalazimika kusema kwa uaminifu kuwa vitabu hivi viwili havielezi kabisa daraja hiyo bora ya kutoa haki. Tuvitazamieje vitabu hivyo viwili kwa daraja hiyo ya tatu, hata daraja ya kwanza na ya pili pia haikuelezwa humo kwa ukamilifu. Kwani, kwa kuwa Torati ilishuka kwa ajili ya Mayahudi tu na Hadhrat Masihi naye alitumwa kwa kondoo tu wa wana wa Israeli, basi hivyo vilihusikanaje na wengine hata wangelitolewa maagizo ya adili na hisani yanayowahusu! Kwa hiyo, amri zile zote zikakoma mpaka kwa wana wa Israili pekee. Kama haikukoma mpaka kwao, kwa nini, basi, Yesu ingawaje alisikia kilio cha mwanamke mmoja na ombi lake la kujinyenyekeza likamfikia, hata hivyo Yesu hakumhurumia, bali akasema mimi nimetumwa kwa wana wa Israeli tu. Basi, kama Yesu mwenyewe

hakuonyesha kimatendo mfano wa huruma kwa wengine wasiokuwa wana wa Israeli, iweje tutegemee kuwa ndani ya mafundisho ya Yesu mna amri ya kuwahurumia watu wa mataifa mengine. Yesu alisema wazi wazi kuwa mimi kamwe sikutumwa kwa mataifa mengine. Sasa je, tunaweza kutumaini kwamba katika mafundisho ya Yesu kuna maagizo kadha kuwahurumia watu wa mataifa mengine? Hapana, bali mafundisho ya Yesu yanahusikana na Mayahudi tu, na Yesu mwenyewe alikuwa hajioni kuwa na madaraka ya kuwatolea maagizo watu wa mataifa mengine, basi angewezaje kutoa mafundisho ya rehema kwa watu wote. Hata kama yameandikwa katika Injili maneno yaliyo kinyume na maneno haya ya Yesu kwamba mafundisho yangu na huruma yangu yakoma mpaka kwa Mayahudi tu, bila shaka hiyo itakuwa nyongeza ya baadaye, kwani hairuhusiwi hitilafu baina ya manano mawili ya mtu.

Kadhalika, Torati nayo ilikusudia Mayahudi pekee na mafundisho yote ya Torati yalikoma mpaka kwa Mayahudi tu. Lakini ile kanuni ya uadilifu na hisani na huruma kwa wanadamu wote iliyokuja duniani ndiyo Kurani peke yake. Mwenyezi Mungu Anasema:

قُلْ يَاأَيُّهَا النَّاسُ إِنِّي رَسُولُ اللَّهِ إِلَيْكُمْ جَمِيعًا[30]

[30] Al-A‘raaf 7:159

Yaani, sema enyi watu, mimi nimetumwe nikiwa Mtume kwenu nyote. Tena Akasema:

وَمَآ اَرْسَلْنٰكَ اِلَّا رَحْمَةً لِّلْعٰلَمِيْنَ ○[31]

Yaani, tumekutuma kwa kuwarehemu walimwengu wote.

[31] Al-Anbiyaa 21:108

## Swali la nne

Masihi amesema maneno haya kujihusu: 'Njooni kwangu enyi mliochoka nami nitawapumzisha', na kwamba, 'Mimi ni nuru, na mimi ni njia, mimi ni uhai na ukweli'. Je, mwanzilishi wa dini ya Kiislam aliwahi kusema popote maneno hayo au maneno kama hayo kwa ajili yake mwenyewe?

**Jibu:** Katika Kurani Tukufu imesemwa kwa uwazi:

قُلْ إِن كُنتُمْ تُحِبُّونَ اللَّهَ فَاتَّبِعُونِي يُحْبِبْكُمُ اللَّهُ[32]

Yaani, waambie kwamba ikiwa nyinyi mwampenda Mungu, basi njooni mnifuate, ili Mungu pia Awapendeni na Asamehe dhambi zenu. Ahadi hii kwamba kwa kunifuata mimi, mtu anakuwa mpendwa wa Mungu, inashinda maneno ya Masihi yaliyotajwa juu, kwani hakuna daraja kubwa kuliko mtu kuwa mpendwa wa Mungu. Basi, nani ana haki zaidi ya kujiita nuru kuliko yule ambaye kufuata njia yake humfanya mtu kuwa mpendwa wa Mungu! Kwa hiyo Mungu mwenye shani, Amempa Mtume s.a.w. jina la '*NURU*'. Katika Kurani Tukufu kama Anavyosema:

قَدْ جَاءَكُم مِّنَ اللَّهِ نُورٌ[33]

---

[32] Aali'Imraan 3:32

[33] Al-Maaida 5:16

Yaani, imewajieni nuru ya Mungu. Na sentensi hii, 'Enyi mliochoka, njooni kwangu nitawapumzisha', yaonekana haina maana. Ikiwa maana ya kupumzisha ni raha ya dunia na ruhusu ya kufanya upendavyo bila kizuizi, basi sentensi hiyo bila shaka ni sahihi. Maana, mtu anaposilimu anapaswa kusali sala tano kila siku. Anapaswa kuamka asubuhi na mapema kwa kusali sala ya alfajiri kabla jua halijachomoza; yampasa kutawadha kwa maji hata maji yakiwa baridi namna gani katika siku za baridi. Tena hana budi kukimbilia msikitini mara tano kwa ajili ya sala ya jamaa. Na kisha usiku karibu saa tisa anapaswa kuamka kutoka katika usingizi mzito na kusali sala ya Tahajudi. Yampasa kujiepusha kutazama wanawake wageni. Anapaswa kujitenga na kunywa pombe na kila kilevyacho. Anapaswa kutunza haki za watu kwa kuogopa kuhukumiwa na Mungu. Na anapaswa kufunga saumu sawa na amri ya Mwenyezi Mungu kila mwaka kwa siku thelathini au ishirini na tisa mfululizo. Anapaswa kutekeleza ibada zote za kifedha kimwili na za kiroho. Lakini Mwislamu mwenye bahati mbaya akiritadi na kuwa Mkristo, papo hapo anatupilia mbali mizigo yote hii toka kichwani mwake, na anajishughulisha kulala, kula, kunywa pombe na kuustarehesha mwili wake, na mara moja anaziacha amali zote ngumu, na kama wanyama, hana shughuli nyingine isipokuwa kula, kunywa na kushughulikia mambo machafu ya anasa.

Basi, kama maneno ya Yesu yaliyo hapo juu yanamaanisha hii tu kuwa mimi nitawapumzisha bila shaka twakubali kwamba Wakristo wana raha sana katika maisha haya duni ya siku chache kwa sababu ya kutenda wapendavyo pasipo mipaka hata kwamba hakuna mfano wao duniani. Wanaweza kama nzi kujikalia kitu chochote. Nao kama nguruwe, wanaweza kula kila kitu. Mabaniani hawali nyama ya ng'ombe na Waislamu hawali nyama ya nguruwe, lakini hao waroho hutafuna hizo zote mbili. Ni kweli: 'Kuwa Mkristo ukafanye chochote utakacho'. Ndani ya Torati nguruwe ameharimishwa kwa kukazania na kusisitiza sana, hata kumgusa pia ilikuwa mwiko, na iliandikwa wazi wazi kuwa uharamu wake ni wa kudumu. Lakini watu hao hawakumwacha hata nguruwe pia aliyechukiwa na Manabii wote. Haya, tumekubali Yesu kuwa mlevi, lakini, je, aliwahi kula nyama ya nguruwe pia? Bali, yeye katika methali moja nasema, 'Msitupe lulu zenu mbele ya nguruwe'. Basi, ikiwa lulu zamaanisha maneno matakatifu, muradi wa nguruwe ni watu wachafu. Katika methali hii Yesu anashuhudia bayana kwamba nguruwe ni mchafu, kwani, kifananishwacho na kitu fulani, hakina budi kilingane na hicho.

Ilimuradi, starehe waliyopatiwa Wakristo ndiyo starehe ya kufanya chochote bila kujizuia na kujihalalishia hata kilichokatazwa, lakini raha ya

kiroho inayopatikana kwa kuungana na Mungu, nanena kwa kupaza sauti kwamba watu hao hawakubahatika kuipata hata kidogo. Machoni pao kuna mapazia, na mioyo yao imejifia na imo gizani. Watu hao wameghafilika kabisa na Mungu wa kweli, na wamemchukulia bila haki mtu mnyonge asiye kitu mbele ya Yule Aliye wa milele kuwa Mungu. Ndani yao hamna baraka, hawana nuru ya moyo, hawana mapenzi ya Mungu wa kweli, bali hata hawamtambui Mungu wa kweli. Hamna baina yao yeyote, naam, hamna hata mmoja, ambaye anazo alama za imani. Kama imani ni baraka kweli, bila shaka alama zake zapaswa kuwepo; lakini yuko wapi Mkiristo mwenye alama zilizoelezwa na Yesu? Basi ama Injili inasema uongo au Wakristo ndio waongo. Angalieni, alama za waaminio ilizoeleza Kurani Tukufu zinapatikana katika kila zama. Kurani Tukufu inasema, mwamini hupokea ufunuo, mwamini husikia sauti ya Mungu, maombi ya mwamini hukubaliwa zaidi sana kuliko wote, mwamini hudhihirishiwa habari za ghaibu, mwaminio husaidiwa na misaada ya kimbingu. Basi, jinsi alama hizo zilivyopatikana zamani ndivyo zinavyopatikana kama kawaida hata sasa pia. Hii inathibitisha kuwa Kurani Tukufu ni Neno Takatifu la Mungu, na ahadi za Kurani ni ahadi za Mungu. Inukeni, Wakristo! Shindaneni nami kama mna uwezo. Kama mimi ni mwongo, nichinjeni basi, waila nyinyi mko chini ya lawama ya Mungu, na nyayo

zenu zinakanyaga moto wa jahanamu. Na amani iwe juu ya afuataye mwongozo.

Mwandishi,
Mirza Ghulam Ahmad
wa Qadian,
Wilaya ya Gurdaspur,
22 Juni, 1897